SUPA JACKPOT
TZS.1,065,505,647
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4

## TMA yatoa hadhari mvua kubwa ya siku 5


Vyama vinapochekelea uhuru mikutano, vianze na kutii angalizo
siasa
Taliban kundi kandamizaji kwa wanawake, wasichana
Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU
UJIO MIKUTANO
Vyama visiwe muuaji maendeleo demokrasia

UKURASA 11

Jumatano Januari 11, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581187
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Samia aonya UVCCM siasa za uhasama

UKURASA 2



Mwenyekiti wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akipokea Bendera ya Taifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Mkoa wa Mara, Mary Daniel, ikiwa ni ishara ya kuhitimisha matembezi ya UVCCM wakati wa shamrashamra za kuadhimisha Miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kijiji cha Paje, Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: IKULU**



## Wanafunzi wasomea chini ya mti madarasa yakiezuliwa paa

UKURASA 8

Mwalimu wa Shule ya Msingi Butibu, Halmashauri ya Ushetu, mkoani Shinyanga, Catherine Kagenzi (kulia), akiwafundisha wanafunzi wa darasa la pili. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Watumishi matatani madai wizi mifuko 1,900 mbolea ya ruzuku

UKURASA 4

UKURASA WA 2

### MWINYI ASAMEHE WAFUNGWA 20 Z'BAR KUTUMIKIA TAIFA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametoa msamaha kwa wafungwa 20 waliokuwa wanatumikia adhabu zao, kwenye Chuo cha Mafunzo...

UKURASA WA 3

### MAHAKAMA YAKUBALI OMBI LA SUGU, MSIGWA KUFICHA MATOKEO VIPIMO VVU KWA WAFUNGWA

MAHAKAMA Kuu Masjala Kuu, imetupilia mbali ombi lililowasilishwa na waliokuwa wabunge wa Chama...

UKURASA WA 5

### GONDWE: WANAFUNZI SEKONDARI WASIO NA SARE WAVAE ZA MSINGI



MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, ameagiza wanafunzi wote waliofaulu kwenda sekondari kwenye wilaya yake ambao

MICHEZO SIMBA KUVAANA NA CSKA MOSCOW UK. 24 KATUNI UK. 6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akishiriki kwenye mnada wa samaki katika Diko na Soko la Samaki Malindi, Wilaya ya Mjini Unguja jana, wakati dalali wa soko hilo, Ali Hassan Mchoro, akimnadi samaki aina ya jodari, Mke wa Rais, Mama Mariam Mwinyi (kushoto), alimnunua kwa bei ya 95,000/-. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi asamehe wafungwa 20 Z'bar

**Na Christina Mwakangale**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametoa msamaha kwa wafungwa 20 waliokuwa wanatumikia adhabu zao, kwenye Chuo cha Mafunzo (Magereza) kati yao 11 kutoka Unguja na tisa Pemba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Idara ya Mawasiliano Ikulu-Zanzibar, Charles Hilary, hatua ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, inatokana na Kifungu cha 59 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.

Taarifa hiyo ilisema kifungu hicho kinampa Rais mamlaka ya kutoa msamaha kwa mtu aliyehukumiwa kwa kosa lolote na kwa kutumia uwezo aliopewa kikatiba.

"Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kusherehekea miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar, amewapatia msamaha kwa kuwaachia huru jumla ya wafungwa 20.

"Wanafunzi hao ni wanaotumikia adhabu zao Chuo cha Mafunzo (Magereza) ambapo kati ya hao wanafunzi 11 kwa Unguja na wanafunzi tisa kwa upande wa Pemba," ilisema taarifa hiyo.

Pia iliongeza kwamba, hatua hiyo ni kawaida kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kutoa msamaha kwa baadhi ya wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo katika kuadhimisha kumbukumbu hizo.

# Samia aonya UVCCM siasa za uhasama

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka vijana wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wanachama wa chama hicho kufanya siasa za kistaarabu ili kuepuka malumbano wanapokuwa kwenye majukwaa ya kisiasa.

Amewataka kujibu hoja kwa ushahidi na takwimu ili wasionekane wanabwabwabwaja.

Alitoa wito huo jana mjini Unguja, wakati akihutubia hafla ya kilele cha matembezi maalum ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), ya kuadhimisha miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Wanasema ukisema kwa ustaarabu na kuchagua ya kusema wewe unajiamini na kama unajiamini huna haja ya kupayuka unajibu hoja yako kwa kujiamini na kwa ushahidi, lakini unapobwabwaja na kupayuka ni ishara ya woga, alisema na kuongeza:

"Niwaombe sana msiende kupayuka naomba mkaitumie fursa ya mikutano ya hadhara nendeni kajibuni hoja na kueleza yale serikali yenu iliyoyafanya."

Alibainisha kuwa CCM imejipanga vyema huku akisisitiza kisijiingize kwenye mtego wa vyama ambavyo havijajipanga.

Aliwaomba wana CCM wanapokosolewa kuyaangalie yale ya kweli wayachukue na kuyafanyia kazi kwa kuondoa makosa na yale ambayo sio ya kweli waende kujibu hoja huku akitaka kuzingatia ustahimilivu.

Alisema kutokuwa na ustahimilivu mmoja atakapopandishwa kwenye jukwaa hatokwenda kujibu hoja badala yake atapayuka na kuwataka vijana kujipanga.

Rais Samia ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Taifa, alisema watakapokuwa wanakosolewa na kurekebisha yaliyokosolewa, ni muhimu kufanya mabadiliko ndani ya chama na kuacha mwelekeo wa kila siku bali warudi kuwa wamoja kama chama kinachoongoza nchi.

"Turudi tuwe chama kiongozi wengine wale wote tuliwazaa sisi, kwahiyo tuonyeshe kwamba sisi ni wazazi na sisi ni kiongozi wa siasa ndani ya nchi hii," alisema na kuongeza:

"Utakapokwenda kupayuka na kujibu hoja za ovyo hapo huonyeshi uongozi, uongozi ni kuonyesha njia, twendeni tukaonyeshe njia kwa wengine."

"Ni kawaida kama atakuja mtu atakutukana na hujibu mwisho atakaa kitako na kujitathmini na kusema mbona ninayemchokoza hachokozeki nadhani ninakasoro, atarekebisha kasoro yake," alisema Rais Samia.

"Niwaombeni sana twendeni tukafanye mabadiliko ndani ya chama na jumuiya zetu, yale tuliyoyazoea maugomvi kati yetu yakaachwe, yakakome, tunakwenda kwenye mapambano ya kisiasa kutetea nafasi yetu ndani ya nchi hii," alisisitiza Rais Samia.

"Twendeni tukiwa tunajiamini, tumejitayarisha na tukiwa tumebadilika sio wale wale, huyu kamchokoza huyu, huyu anakundi hili, hatutafika ndugu zangu, 2024 tuna uchaguzi wa serikali za mitaa tukienda tumegawanyika hatutafanya vizuri, twendeni tukiwa wamoja," alisisitiza Rais Samia.

Alisema wakishabadilika watapaswa kujenga mpya nchi na kwamba yale makandokando yaondolewe, akisisitiza kuwa zama za ugonvi, kupigana na kutukanana katika siasa sasa ziishe na waende na hoja za maana za kujenga.

Rais Samia aliwataka wavumiliane na kuleta maendeleo ya kweli na yenye tija, ili wajenge Tanzania mpya yenye maendeleo endelevu na kwamba taifa linahitaji kutunza na kuendeleza amani na mshikamano, ili muungano wao uwe imara kwa hatua zaidi za kimaendeleo.

Rais Samia alisisitiza vijana na Watanzania kwa ujumla kuendeleza kuilinda amani ya Tanzania, akisema ni jambo muhimu ambalo wanatakiwa kulifanyia kazi.

**AJIRA**

Kuhusu ajira amesema kazi ya serikali sio kutengeneza ajira, bali ni kuweka mazingira mazuri ili vijana wayatumie.

Aliyasema hayo jana mjini Zanzibar, wakati akihutubia wanachama wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), katika hafla ya kilele cha matembezi maalum ya kuadhimisha Miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aliwasisitiza vijana kwenda kutengeneza ajira kwa mazingira yaliyokuwapo, akieleza kuwa wa sasa wanakimbilia kutaka utajiri wa nyumba na gari zuri na baada ya muda utajiri walioutaka kwa haraka unawapiga kwa kushindwa kuhudumia makazi au usafiri walionao.

"Jana nilikuwa naangalia televisheni Watanzania wanahojiwa kuhusu ajira, kila anayemaliza anasema serikali itengeneze ajira, nataka kuwaambia kazi ya serikali si kutengeneza ajira, bali ni kuweka mazingira mazuri ili vijana muyatumie kutengeneza ajira na hiyo kazi tunaifanya yja kutosha," alisema Rais Samia.

Pia aliwataka vijana kutengeneza ukwasi, akimaanisha kujiwekea utaratibu wa kujipatia fedha kila wakati, huku akiwataka kuwa na miradi midogo midogo na kazi ya serikali ni kufanya makusanyo makubwa na kutekeleza miradi inayotelekezwa.

"Fursa zipo kwenye uchumi wa buluu kwa mfano visiwa vya Zanzibar Mungu ametuzungusha pwani na bahari, lakini tumeshafanya uvuvi tumeshaitumia bahari na pwani toka dunia hii imeumbwa kiasi kwamba sasa pwani zetu zimebakia na rangi za kupendeza tu, lakini hazina rasilimali kwasababu tulishavuna na kuharibu mazingira," alisema Rais Samia.

Kadhalika, alisema kuna miradi ambayo vijana wangeweza kufanya ndani ya pwani ambayo ingewawezesha kuchuma fedha kila wakati, akitolea mfano uvuvi wa vizimba, ikiwa ni miongoni mwa miradi ambayo alielekeza ufanyiwe kazi.

Aidha, alimpongeza Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi, kwa kutenga fedha za kuwaunga mkono vijana katika kazi za namna hiyo, akiahidi kuwa endapo vijana watajipanga na kuja na mawazo mazuri fedha za kuwasaidia kuanza miradi yao zipo, akionesha kutoridhishwa na tabia ya kuwa na aina moja ya miradi kila siku.

"Ukiona mtu kafungua duka au saluni utaona kila eneo ni hivyo hivyo hujui nani atanunua, mje na mawazo mapya ambayo mahitaji ya soko lipo na mnaweza mkatengeneza pesa, mkiweza kufanya hivyo vijana mmeweza kutengeneza uchumi katika ngazi ya chini," alisema Rais Samia.

"Fedha zitakuwa zinazunguka huko, kelele za ukosefu wa ajira zitakuwa hazipo, uchoshaji wa kwenda pahali unakuta vijana wamechoka, unaambiwa Mama umekuja basi fanya kitu tupone mimi nikikuponyesha wakati huo muda mwingine nani anakuponyesha? Nendeni jipangeni, jitumeni mpate fedha zenu," alisema Rais Samia.

**KILIMO**

Rais Samia alisema kilimo ni sehemu nyingine ambayo vijana wanaweza kuitumia kama fursa ya kujitengenezea fedha, akieleza kuwa wanakokwenda kuna tatizo la upungufu wa chakula na kwamba wanaweza kuzalisha mboga, chakula, nyama na kila kitu kwa wingi na wakajitosheleza na hata kuuza kwa wengine.

Aidha, alitoa wito kwa vijana kwenda kujenga uchumi wa chini na kuisaidia serikali, akisisitiza ubunifu na weledi wa kutumia rasilimali zilizoko na kwamba mapinduzi ya kiuchumi na ustawi wa jamii bado ndio mapambano ambayo wanaendelea nayo.

***Imeandikwa na Maulid Mmbaga (DAR) na Rahma Suleiman (Zanzibar).**

HABARI KITAIFA

# Mahakama yakubali ombi la Sugu, Msigwa kuficha matokeo vipimo VVU kwa wafungwa

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masjala Kuu, imetupilia mbali ombi lililowasilishwa na waliokuwa wabunge wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Joseph Mbilinyi na Peter Msigwa, wakilalamikia kifungo cha upweke, chakula na wafungwa kupekuliwa wakiwa utupu mbele za wengine.

Hata hivyo, imekubali hoja ya vitendo vya kuwalazimisha wafungwa kupima Virusi vya Ukimwi (VVU) na kutoa matokeo kwa watu watatu ni kuwakosea wafungwa haki ya utu, faragha na uhuru.

Hukumu hiyo ilitolewa hivi karibuni na jopo la majaji watatu, Jaji Elinaza Luvanda, Edwin Kakolaki na Ephery Kisanya.

Jopo hilo lilisema katika uamuzi wake waleta maombi walishindwa kutoa ushahidi wa kutosha kuthibitisha hoja nane kati ya tisa za kupinga uhalali wa Sheria ya Magereza inayohusu mwenendo wa mambo ya wafungwa wakiwa gerezani.

"Suala la kwanza tuligundua vitendo vya kuwalazimisha wafungwa kupima VVU na kutoa matokeo kwa watu watatu ni kuwakosea wafungwa haki ya utu, faragha na uhuru iliyoainishwa chini ya Ibara ya 12(2) na 1.6(1) ya Katiba, malalamiko mengine yote yametupiliwa mbali," lilisema jopo.

Wakati wa usikilizwaji wa ombi hilo, walalamikaji walilalamikia vitendo vya Jeshi la Magereza kuwapima wafungwa VVU kwa lazima wanapoingia gerezani na kutoa matokeo hadharani kitendo walichodai ni kinyume cha Katiba.

Pia waleta maombi walilalamikia upekuzi wa kihuni na usio na heshima kwa wafungwa kwa kuwavua nguo na kubaki utupu mbele ya watu wengine na kutoa jozi moja ya sare kwa wafungwa bila mavazi mbadala.

Waombaji walikuwa wakipinga msongamano gerezani na uhaba wa vifaa vya kulalia, kuwashirikisha wafungwa katika kazi bila malipo ya ujira, vifungo vya upweke kwa kunyimwa kutembelewa na utoaji wa mlo chini ya kiwango kilichopendekezwa.

Majaji hao walisema hakuna sheria inayoruhusu upekuzi huo kwa namna iliyoonyeshwa na waleta maombi kuwa wafungwa wanalazimika kuandamana wakiwa bila nguo, upekuzi usio na heshima katika miili yao, ikiwa ni pamoja na sehemu za siri, kulazimishwa kujisaidia kwenye ndoo.

> **"Suala la kwanza tuligundua vitendo vya kuwalazimisha wafungwa kupima VVU na kutoa matokeo kwa watu watatu ni kuwakosea wafungwa haki ya utu, faragha na uhuru iliyoainishwa chini ya Ibara ya 12(2) na 1.6(1) ya Katiba, malalamiko mengine yote yametupiliwa mbali," lilisema jopo.**



"Sheria kama ilivyo, inataka kupekuliwa kwa heshima, adabu kwa kuzingatia heshima na faragha, matumizi mabaya tu ya madaraka hayafanyi kile kilichotolewa katika Sheria ya Kudumu ya Magereza kuwa kinyume cha Katiba.

"Sheria inayosimamia upekuzi wa wahalifu au wafungwa wanapoingizwa gerezani iko sawa na inatoa ulinzi wa kutosha kuhusiana na namna ya upekuzi wa heshima na staha unavyopaswa kufanywa.

"Iwapo kuna tabia za maofisa wa Magereza zinazokiuka sheria ya uendeshaji wa upekuzi, tunaona huo unaweza kushughulikiwa kiutawala," walisema majaji hao katika hukumu yao.

"Ushahidi kuhusu malalamiko ya mateso, adhabu ya kinyama au ya kudhalilishwa katika kifungo cha upweke haupo.

"Kuhusu malalamiko ya utoaji wa chakula na mlo kwa wafungwa chini ya kiwango kilichopendekezwa, walisema wafungwa hawapatiwi matunda au mboga za majani kama sehemu ya 'menu' yao kuu, au mihogo, viazi kama sehemu ya kifungua kinywa, hawakutoa ushahidi wowote.

"Walalamikaji walikuwa na wajibu wa kutoa maelezo ya kutosha kwa mahakama kuchunguza uhalali wa Katiba ya sheria inayolalamikiwa.

"Haitoshi kwa walalamikaji kudai na kisha kukimbilia mahakamani kuomba itamke kifungu fulani cha sheria kuwa ni kinyume cha katiba bila ushahidi wa kuthibitisha kwamba kweli kuna uvunjifu."

Majaji hao walisema mahakama inaona kuwa katiba ni hati nzito na haiwezi kutumika katika jambo lisilo la maana.


# NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED, NGOMENI ENTERPRISES, JADA INVESTMENT LIMITED** na **MANGWEMBE 2011 COMPANY LIMITED** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED**, tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | HP PLANNERS AND EVENTS MANAGEMENT LIMITED | PETER DANIEL SHEMBIRU | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI No.KND002948, ARDHI No. KND/KIN/KSH7/23 | KINONDONI SHAMBA, WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 30/01/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | NGOMENI ENTERPRISES |
| 2 | MAGORI MWITA CHACHA | MAGORI MWITA CHACHA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | YANGEYANGE MSONGOLA WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 28/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 3 | EMMANUEL ANAEL UWISO | EMMANUEL ANAEL UWISO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | TEGETA 'A', WILAYA YA UBUNGO, DAR ES SALAAM | 27/01/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LIMITED |
| 4 | ROBERT WILSON SALIJA | ROBERT WILSON SALIJA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI No.130026, PLOT No. 1323, BLOCK 'A'. | MBEZI, KIVUKONI WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 28/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JADA INVESTMENT LIMITED |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED, P. O. Box 62163, Dar es Salaam**
**Tel: 0658100737, 0757276263**
**Email: amazauctionma@gmail.com**

**MANGWEMBE 2011 COMPANY LIMITED**
**P. O. Box 12943, Arusha**
**Tel: 0752 632 033, 0628 512 033**
**Email: mangwembe@gmail.com**

**NGOMENI ENTERPRISES**
**P. O. Box 36359, Dar es Salaam**
**Tel: 0719974916, 0784252048**
**Email: ngomenienterprises@gmail.com**

**JADA INVESTMENT LIMITED**
**P. O. Box 69098, Dar es Salaam**
**Tel: 0788493699, 0768085727**
**Email:**

17222302

# TMA yatabiri mvua siku tano mfululizo

Na Elizabeth Zaya

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA), imetoa tahadhari ya hali ya hewa mbaya na uwapo wa vipindi vya mvua kubwa kwa siku tano mfululizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na TMA, mvua kubwa zinatarajiwa kukumba maeneo ya mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara, Tanga, Pwani, Dar es Salaam na visiwa vya Unguja na Pemba.

Pia TMA ilisema katika kipindi hicho cha tahadhari ya uwapo wa vipindi vya mvua, upo uwezekano wa kutokea athari za wastani.

Imetaja athari zinazoweza kujitokeza kuwa ni pamoja na baadhi ya maeneo kuzungukwa na maji pamoja na ucheleweshwaji wa shughuli za uchumi na usafirishaji.

TMA iliwataka wananchi kuchukua tahadhari katika kipindi chote.

Septemba, mwaka jana, TMA ilitoa utabiri wa msimu wa mvua za vuli kwa maeneo yanayopata mara mbili kwa mwaka yatapata misimu miwili ya mvua za chini ya wastani.

Kwa mujibu wa taarifa ya TMA ya Septemba mwaka jana, pia kunatarajiwa kuwapo na mwendelezo wa mvua kwa mwezi Januari, mwaka huu.

Kadhalika, taarifa hiyo ilieleza matarajio ya vipindi vya joto kali kuliko kawaida katika msimu wa vuli maeneo ya Kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba, Arusha, Manyara na Kilimanjaro.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiungana na wanafunzi wa Shule ya Msingi Kiwani, wakati wakiimba wimbo wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, baada ya kufungua Kituo cha Afya Daraja la Pili cha Kendwa, Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba jana, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za maadhimisho ya Miaka 59 ya Mapinduzi hayo. **PICHA: OMR**

# Watumishi 4 mbaroni wakituhumiwa wizi mifuko 1,900 mbolea ya ruzuku

Na Thobias Mwanakatwe

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe limewatia mbaroni watumishi wanne wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kwa tuhuma za wizi wa mifuko 1,900 ya mbolea ya ruzuku iliyotolewa na serikali.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songea, Rashid Ngonyani, katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari, alisema kati ya watumishi hao, watatu ni kutoka Idara ya Kilimo na mmoja ni mwalimu.

Kukamatwa kwa watumishi hao kumekuja siku chache baada ya Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe kueleza Mkoa wa Songwe unaongoza nchini kwa kuhujumu mbolea ya ruzuku.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Aloyce Madaraka ambaye ni Ofisa Mwandamizi Idara ya Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, anayedaiwa kudanganya ana shamba la ekari 30 na kujipatia mifuko 71 ilhali hana shamba.

Alisema mtuhumiwa huyo pia amewaingizia watu wengine taarifa za uongo na kuchukua mbolea hiyo.

Wengine ni Anton Buyongera ambaye ni Ofisa Kilimo, Kata ya Iyula, Wilaya ya Mbozi taarifa zimeonesha ameingiziwa mifuko 855 na baada ya kuhojiwa alikana kupokea mifuko hiyo na kusema hana shamba.

Mtuhumiwa wa tatu ni Rehema Mwandulusya, Ofisa Kilimo, Kata ya Ilolo, wilayani Mbozi, anayehusishwa na utoaji wa mifuko 600 kwa kushirikiana na mtu ambaye jina lake halikutajwa ambaye anaendelea kutafutwa na Jeshi la Polisi.

Mtumishi mwingine anayeshikiliwa na jeshi hilo ni James Ngunda, anayedaiwa kudanganya ana shamba lenye ekari 200 na kujipatia mifuko 400.

Alisema baada ya uchunguzi ameonekana kutokuwa na shamba.

Kaimu Kamanda Ngonyani, alisema baada ya mahojiano ya awali watuhumiwa hao wamekiri kujihusisha na wizi huo kupitia mfumo wa utoaji wa mbolea ya ruzuku.

"Wote hawa tunawashikilia kwa makosa ya uhujumu uchumi kwani wamebainika kudanganya kwa kuingiza taarifa za uongo kwenye mfumo na kujipatia mbolea ya ruzuku ambayo wao wameenda kuiuza kusikojulikana," alifafanua Kamanda Ngonyani.

## Bashe ataja mikakati kukuza kilimo nchini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imeweka mikakati ya kukuza sekta hiyo, ikiwamo kuchimba mabwawa 14 ya maji kwa ajili ya umwagiliaji yenye uwezo wa kuzalisha ujazo lita milioni 131.

Mkakati mwingine ni ifikapo 2030, serikali inakoma kuagiza sukari nje na kupunguza kiasi cha mafuta ya kula kinachoingizwa nchini.

Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wahariri na waandishi wa habari katika warsha ya usalama wa chakula inayoendelea jijini hapo.

Alisema mabwawa hayo yamechimbwa katika mikoa tofauti kwa ajili ya kuboresha kilimo cha umwagiliaji nchini.

"Tumejipanga kuhakikisha kilimo kinasonga mbele hasa ukizingatia serikali imetoa kipaumbele kwenye bajeti ya wizara," alisema.

Akizungumzia uzalishaji wa mahindi, alisema nchi inazalisha tani 17, lakini mahitaji ya chakula ni tani 13 hadi 15 na kuhakikisha hakuna upungufu wa chakula nchini.

"Tuko vizuri kwenye kuimarisha kilimo, tunazidi kusonga mbele kuhakikisha kinapiga hatua kubwa ifikapo 2030," alisisitiza.

Alisema kilimo ni uti wa mgongo na kinapaswa kusimamiwa vizuri ili kiweze kupiga hatua katika maeneo mbalimbali nchini.

Kadhalika, ifikapo 2030 wanahitaji kuona kilimo kimefika mbali na kuachana na cha mazoea.

Akizungumzia zao la pamba, alisema wanaenda kwenye vijiji kuhamasisha kilimo hicho kwa kuwa ni zao la biashara.

Pia ujenzi wa vihenge na maghala ni kwa ajili ya kuongeza uwezo wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), kuhifadhi chakula tani 251,000 hadi 501,000.

Alisema kupitia mradi wa sumukuvu, jumla ya maghala 14 yamejengwa kwa ajili ya kuhifadhia mazao yanapotoka shambani kuvunwa.

Maghala hayo alisema yatasaidia kuepusha sumukuvu kwa wananchi kutokana na sehemu ya kuhifadhia chakula kuwa na usalama zaidi.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Andrew Masawe, aliwashukuru wanahabari wa taarifa za uelimishaji ikiwamo kuhabarisha sekta ya kilimo kwa weledi.

Hata hivyo, alisema baada ya semina hiyo anaamini ushirikiano utaimarika zaidi ili kuipeleka mbele sekta hiyo nchini.

**"Tumejipanga kuhakikisha kilimo kinasonga mbele hasa ukizingatia serikali imetoa kipaumbele kwenye bajeti ya wizara," alisema.**

## 'Changamkieni fursa kuona madaktari bingwa'

**Na Halfani Chusi**

KATIBU wa Afya Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala, Rajabu Kaseke, amewataka wakazi wa Dar es Salaam, kujitokeza kwa wingi hospitalini hapo kukutana na madaktari bingwa wa fani mbalimbali ili waweze kupimwa afya na kupatiwa ushauri na tiba.

Kaseke alitangaza kuwapo kwa fursa hiyo jana mkoani Dar es Salaam, kwenye hafla ya uzinduzi wa kambi ya siku nne ya matibabu inayoshirikisha madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Muhimbili-Mloganzila na Mwananyamala.

Alisema lengo la kuzindua kambi hiyo ni kubadilishana uzoefu wa kitabibu kupitia agizo la Wizara ya Afya linalohimiza hospitali za juu kushirikiana na hospitali za chini.

Alibainisha kuwa kambi hiyo itajikita kutoa elimu ya afya na tiba kwenye magonjwa ya lishe akikumbushia kuwapo kwa tatizo kubwa la magonjwa yasiyoambukiza kutokana na ukosefu wa elimu hiyo.

"Tunawaomba wananchi wachangamkie fursa hii, wajitokeze kwa wingi waweze kukutana na madaktari bingwa ambao watakuwapo hapa kwa wiki hii yote isipokuwa Alhamisi siku ya sikukuu."

"Wapo madaktari bingwa wa magonjwa mbalimbali kama mkojo, moyo, mfumo wa damu, mifupa, magonjwa ya ndani na kuhamasisha wananchi kukata bima ya afya," alisema na kuongeza:

"Huduma hizo zinatolewa kwa gharama ambazo zinawapa wananchi unafuu mkubwa kwa sababu kwenye kambi hii mwananchi anapata fursa ya kumuona daktari bingwa-mbobezi kwa gharama ndogo ya Sh. 3,000 tofauti na utakavyo mfuata hospitalini kwake."

Aidha, alisema hospitali hiyo inakabiliwa na ukosefu wa madaktari bingwa wa moyo, mkojo, mfumo wa damu, pamoja na madaktari bingwa wabobezi.

Mwanahamisi Mohamedi, alisema huduma hiyo imewawezesha kukutana na madaktari bingwa kirahisi na kutatuliwa tatizo sugu lililokuwa likimkabili.

"Kwa mfano daktari bingwa wa mfumo wa damu unamuona kwa Sh. 3,000 hii imetupunguzia gharama, lakini pia hata muda wa kuwafuata kwenye hospitali zao," alisema.

Mkazi mwingine, aliyekuwa maeneo hayo akisubiri huduma alisema kambi hiyo imeleta matokeo chanya na kwamba wengi wamejitokeza kupima afya na kuiomba hospitali hiyo kufanya hivyo mara kwa mara.

# Gondwe: Wanafunzi sekondari wasio na sare wavae za msingi

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, ameagiza wanafunzi wote waliofaulu kwenda sekondari kwenye wilaya yake ambao hawana sare kuripoti shuleni na kuanza masomo kwa kuvaa sare walizotoka nazo msingi.

Akizungumza alipotembelea shule mbalimbali jana kukagua mwenendo wa wanafunzi wanaoripoti shuleni katika wilaya hiyo, alisema ni vyema wanafunzi hao wakatumia sare walizokuwa wakitumia shule za msingi kuliko kukosa masomo.

"Wazazi wote ambao watoto wao wanaingia kidato cha kwanza wasijali, hata kama watoto wao hawana sare za shule, wahakikishe wanaenda shuleni, hatutaangalia kwamba hana sare au nini. Hatuwezi kusubiri mtoto akose masomo, hata kama ana sare zake alizozitumia shule ya msingi aje tu hivyo hivyo na mambo yatakwenda taratibu akiendelea kutumia hizo sare za msingi," alisema Gondwe.

"Haitakuwa jambo jema watoto wamefaulu halafu wanabaki nyumbani kwa sababu eti hawana sare za shule, hatutaki kuona mtoto yeyote anabaki nyumbani kwa sababu hiyo wakati analipiwa ada na Rais Samia Suluhu.

Pia Gondwe alisema kwa shule binafsi, ameagiza zote kuweka mwangalizi wa kike (Matron) katika kila gari la wanafunzi ili kuepusha wanafunzi kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji au ukatili wa kijinsia.

"Kwa shule zote binafsi, Kinondoni tumeamua kwamba zenye mabasi, tumeweka matroni na hayo ni maamuzi ya serikali ya wilaya na lengo ni kutengeneza mazingira mazuri kwa watoto kutopata athari za mashambulizi au unyanyasaji wa kijinsia.

"Tusingependa yale yaliyotokea mwaka jana yatokee mwaka huu, nimeshaunda timu tayari ikijumuisha madawati ya jinsia kutoka Jeshi la Polisi na Maofisa Ustawi wa Maendeleo ya Jamii, kwa pamoja watapita shule zote kuhakikisha mabasi yote ya watoto yana matroni kule ndani.

"Lengo letu tunataka kila mzazi anapokabidhi mtoto anajua yuko maeneo salama, tunataka maeneo ya shule zetu za watoto mpaka mabasi yanaendelea kuwa salama kwa watoto wetu. Hatutavumilia shule yoyote ambayo kwenye basi itaweka msaidizi wa kiume, tunataka kuepukana na mazingira hatarishi kwa watoto wetu."

Aliwapongeza wanafunzi waliofaulu kuingia kidato cha kwanza katika wilaya yake pamoja na walimu wao.



Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashimu Mgandilwa (katikati), akisalimiana na Mkuu wa msafara wa viongozi na washiriki wa mafunzo kutoka Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC), Brigedia Jenerali Steven Mnkande, wakiwa kwenye ziara ya mafunzo ya siku tano mkoani Tanga jana. Kushoto ni Katibu Tawala wa Mkoa huo, Pili Mnyema. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

## PSSF yahadharisha wastaafu dhidi ya matapeli

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umetoa tahadhari kwa wanachama wake kuwa makini na matapeli wanaowapigia simu kuwataka watoe fedha ili wapatiwe huduma.

Ofisa Matekelezo Mwandamizi wa Mfuko huo, Amina Mtingwa, ametoa tahadhari hiyo katika banda la PSSSF kwenye Maonesho ya Tamasha la Tisa la Biashara linaloendelea kwenye viwanja vya Maisara ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. "Tunawasihi wanachama wetu wasikubali kupokea maelekezo yoyote kutoka kwa watu wasio wajua kwani huduma zetu zinatolewa bure," alisema Amina.

Pia, alisema wanapokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wanachama wakiwamo wastaafu kuwa wamepigiwa simu na watu waliojitambulisha ni maofisa wa serikali wakitakiwa kutoka fedha ili warekebishiwe mafao yao jambo ambalo sio sahihi.

"Tungewashauri wanachama na wastaafu wetu endapo watahitaji ufafanuzi kuhusu malipo ya mafao mbalimbali wawasiliane na ofisi za PSSSF ambazo zinapatikana mikoa yote Tanzania Bara na Visiwani," alisisitiza.

Alisema mfuko umekuwa ukishirikiana na mamlaka zinazosimamia mawasiliano ili kuwabaini watu hao na kutoa mfano tayari kuna visa 12 vilivyotokea mwezi Desemba, 2022 kuripotiwa kwenye mamlaka husika ili kuwabaini wahalifu hao wa kimtandao.

Akizungumza kuhusu uhakiki wa wastaafu, alisema ni endelevu kila mstaafu anapaswa kujihakiki mara moja kila mwaka.

Kadhalika, Amina alisema mfuko una wastaafu 150,000 ambao hulipwa mafao ya jumla ya Sh. bilioni 60 kila mwezi.

Aliwataka wanachama wa PSSSF walioko kisiwani Zanzibar kutembelea katika banda la mfuko huo ili kuhudumiwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio cha tozo sekta ya utalii kisikike

**JUZI** Chama cha Waongoza Watalii nchini (TATO), kiliiomba serikali kuondoa mkanganyiko wa ukusanyaji wa tozo na kodi katika sekta ya utalii ili kudhibiti upotevu wa mapato unaoendelea kujitokeza maeneo yenye rasilimali za maliasili.

Chama hicho katika mkutano wao uliofanyika jijini Arusha na Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, kilipendekeza serikali kutafuta ufumbuzi wa matatizo hayo ili kuondoa usumbufu, urasimu na upotevu wa mapato unaoendelea kujitokeza kutokana na wingi wa kodi na tozo zinazotokana na utalii, ambazo hukusanywa na Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Chama hicho kilipendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii, kusimamia yenyewe makusanyo yote ya tozo na kodi tofauti na ilivyo sasa, ambapo kuna wizara nyingine mbili zinakusanya.

Kilitoa mfano wa tozo wanazotozwa watalii wanapopita kwenye maeneo ya halmashauri za wilaya, wakati wakiwa njiani kwenda kutazama vivutio mbalimbali katika Hifadhi za Taifa.

Utaratibu huo wa mifumo ya ukusanyaji wa kodi na tozo, unaoendelea kufanywa na taasisi nyingi, umedaiwa kukwamisha na kuchelewesha utekelezaji wa mikakati ya serikali ya kuongeza idadi ya watalii wanaoitembelea Tanzania.

Kwa kweli hoja zilizotolewa na chama hicho ni za msingi kama serikali inataka sekta ya utalii iendelee kukua na kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini bila kupata vikwazo hivyo vya kodi.

Lengo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuitangaza filamu ya Royal Tour, ni kuitangaza Tanzania na vivutio vyake vya utalii ili kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini na kuongeza mapato.

Kama kutakuwa na mkanganyiko huo wa tozo na kodi, kutarudisha nyuma juhudi zote zilizofanywa na Rais za kutangaza vivutio vya utalii.

Chama hicho kilimwomba Rais Samia na serikali yake kuhakikisha masuala yote ya tozo na kodi yanasimamiwa na wizara moja.

Kadhalika, chama kilipendekeza maslahi duni wanayopata waongoza watalii yafanyiwe kazi, wakiwamo wanaopandisha wageni Mlima Kilimanjaro, ambao kwa muda mrefu wamelalamikia malipo ya ujira wa Sh. 5,000 hadi Sh. 10,000 hakilingani na kazi wanayofanya.


Kwa zaidi ya miaka 10 imedaiwa maslahi ya wapagazi katika Mlima Kilimanjaro, hayajafanyiwa kazi, huku wakipendekeza kuongezwa hadi kufikia dola 15 za Marekani, sawa na Sh. 30,000 za Tanzania.

Kutokana na maslahi duni, asilimia kubwa ya waongoza watalii wanakata tamaa ya kuendelea kunufaika na matunda ya utalii na wamekuwa wagumu kutoa mchango wao katika kulinda na kuimarisha rasilimali za utalii wanakuwa wagumu wa kujitolea kukabiliana na majanga ya moto.

Jambo la kufurahisha, waziri mwenye dhamana katika sekta hiyo alisema amepokea mapendekezo yaliyotolewa na wadau wa sekta hiyo, likiwamo la nyongeza ya posho za waongoza watalii na wapagazi kwa siku.

Suala la tozo pia ataliwasilisha katika ngazi zinazohusika ili lifanyiwe kazi na ikiwezekana mwaka ujao wa fedha, lianze kusimamiwa na wizara moja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Miaka 59 ushindi wa Mapinduzi

Na Mwandishi Wetu Zanzibar

**KESHO** Tanzania inaadhimisha miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar, hongera kwa kila Mtanzania na Mzanzibari anayesimama na kutetea uhuru wa taifa hili kuanzia ule uliopatikana mwaka 1961 kwa upande wa Tanganyika na wa mwaka 1964 ambayo ni Mapinduzi ya Zanzibar yaliyoifanya kuwa Jamhuri huru.

Katika juhudi za kumwenzi mfalme wa Mapinduzi ya Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), kilieleza nia yake ya kuanzisha Kiti cha Utafiti (University Research Chair) ambacho kitakuwa cha kwanza kuanzishwa katika historia ya SUZA, kumuenzi Rais wa Kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Abeid Amani Karume.

Kiti hiki cha utafiti kinalenga kumuenzi Karume na kuyaenzi mawazo na fikra zake kwa kuwa miongoni mwa wanaharakati na wanamapinduzi wakubwa waliopambana kwa nguvu zote kuhakikisha Zanzibar na Afrika inakuwa huru ili kujiletea maendeleo kiuchumi, kisiasa, teknolojia na sekta zote za maisha.

Kama kilivyo Kigoda cha Mwalimu Nyerere, cha Karume, kitahifadhi, kuenzi na kendeleza mawazo na fikra zake katika kuleta ukombozi na maendeleo ya Zanzibar, Tanzania na Afrika kupitia utafiti na mijadala mbalimbali ya kisomi kutoka kwa wadau na wataalamu wa utafiti wa kada mbalimbali.

Ni jambo jema kuenzi kazi kubwa za wanamapinduzi ambao walitoa maisha yao kwa ajili ya Watanzania wa Tanganyika na Zanzibar.

Ujio wa Kigoda ni muhimu kwenye kuzienzi, kuzifahamisha na kuzieneza fikra na mawazo ya Karume kwa vijana na jumuiya ya Watanzania hasa zama hizi ambazo ni kama fikra na duru za kizalendo, ukereketwa na mapendo kwa taifa yanaondoka.

Ni nadra kuona vijana wakijitoa muhanga kwa ajili ya nchi yao, tofauti na walivyofanya waasisi wa Tanganyika na Zanzibar, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na Karume. Wapo vijana leo, wataisifu na kuizungumzia timu ya mpira ya Ulaya au Afrika kwa sifa zote lakini ni nadra kukuta vijana hao wakiwazungumzia na kuwasifia waasisi Karume na Nyerere.

Si kwa kingine, ila kwa namna walivyofanya mambo makubwa na kuanzisha fikra na mawazo ya utaifa, umoja, udugu na kulifikisha taifa hapa lilipo leo.

Karume ni mkombozi na mwana maendeleo anayeishi ni mshiriki mkubwa wa kutaka Zanzibar isiyo na umaskini, akijiunga na viongozi wenzake kuwapa Wazanzibari ardhi, kuwajengea nyumba Michenzani, Makunduchi na Gamba Unguja, wakati Pemba zipo Micheweni, Mkoani, Wete na Chake.

Pamoja na hayo anawapatia wananchi maskini ardhi na kuwataka kila kaya kuwa na ardhi ya kulima karafuu ili kujiongezea kipato na kuwa na maisha bora.

Karume ni shujaa wa ukombozi na maendeleo ya nchi hii na Afrika. Karume aliamini kuwaelimisha watu kuwa kila raia apate elimu na kuanzisha utaratibu wa elimu bila malipo, ni mambo ambayo hata sasa yanaishi na vijana wanatakiwa kuyafahamu na kuyaenzi kwa kusoma na kufanikisha ustawi wa taifa kupitia elimu kuanzia ngazi za awali hadi za juu.

Karume amefanya mambo mengi ambayo hata sasa yanaendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na ujasiri wa kutetea wanyonye. Leo Serikali ya Zanzibar na ya Muungano zinaendelea, kupambana na umaskini, kutumia rasilimali kama Bahari ya Hindi kuwekeza kwenye uchumi wa buluu kuwainua watu.

Ni maono ya Karume yanayoonekana sasa SMZ, ikiendelea kupambana na rushwa, kutokuwajibika na matumizi mbaya ya rasilimali za nchi ili kuboresha maisha ya wananchi kwa ubunifu na juhudi kubwa kama walivyofanya viongozi waasisi walioondoa wakoloni na usultan.

Karume wakati wa mapinduzi alifanya mambo yote kwa juhudi kubwa kuondoa wakoloni na usultani, hivyo ni jukumu la Watanzania leo kuendelea kujenga msingi aliouweka kwa kutumia rasilimali zilizoko na kuwainua wananchi kutoka kwenye umaskini na kufikia uhuru kamili na maendeleo.

## TAMISEMI yaja na mfumo mpya ukusanyaji mapato

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imekuja na mfumo mpya wa ukusanyaji mapato wa 'Tausi' ambao utakuwa suluhisho kwa halmashauri zote nchini.

Mfumo umeitwa 'Tausi' kutokana na sifa za ndege huyo kuwa na uwezo wa kugundua hatari na kuzizuia hivyo mfumo huo unaulinzi wa hali ya juu unaozuia mashambulizi ya kimtandao na mengineyo.

Vile vile, alisema sifa nyingine ya Tausi ni kuruka hivyo mfumo huo unamwezesha mtumiaji kutumia simu ya mkononi kupata huduma akiwa sehemu yoyote.

Kuanzishwa kwa mfumo huo kutajibu hoja ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Serikali za Mitaa (LAAC), iliyotaka TAMISEMI kuwa na mfumo mmoja wa ukusanyaji mapato.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, Ramadhani Kailima, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa maofisa wa TEHAMA wa halmashauri na taasisi za serikali yanayoendelea jijini hapo.

Alisema mfumo wa 'Tausi' umeonekana kuwa ni suluhisho baada ya kufanyiwa majaribio kwa halmashauri 54 nchini.

Pia utakuwa wa pekee wa ukusanyaji wa mapato kwa kuwa utakuwa na uwezo wa kusoma makusanyo ya kila halmashauri kwa wakati na kuepusha uvujaji wa mapato.

Alisema mafunzo hayo yatawashirikisha wakurugenzi na wahasibu wa halmashauri na wadau wengine wa serikali.

Aliwataja wadau hao kuwa ni Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Wakala wa Serikali Mtandao.

Taasisi zingine ni Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali, Tume ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Mashtaka Makosa ya Jinai (DCI).

Kadhalika, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuufahamu mfumo huo ili kuwarahisishia katika majukumu yao ya kiutendaji.

Alisema siku ya mwisho ya mafunzo hayo watamwalika Waziri wa TAMISEMI, DCI (Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai), Mkuu wa TAKUKURU na DPP (Mkurugenzi wa Mashtaka) ili wapate taarifa ya mijadala ya mafunzo hayo.

Awali, Mkurugenzi wa TEHAMA wa TAMISEMI, Erick Kitali, alisema mfumo wa kwanza wa ukusanyaji mapato wa LGRCIS ulianza kutumika miaka zaidi ya minane iliyopita na ulionekana na matatizo na wakaanzisha mfumo mpya wa Tausi.

Kitali alisema mfumo huo wa awali utaendelea kuwapo ili kutunza kumbukumbu ya fedha.

Alisema Mkoa wa Dar es Salaam yalifanyika majaribio Desemba mwaka jana ya ukusanyaji mapato na utoaji wa leseni za biashara pamoja na leseni ya vileo za kidijitali ulionyesha mafanikio makubwa.

Alisema wataanza mafunzo wiki ijayo kwa mikoa yote iliyobaki na matarajio ni ifikapo Machi 31, mwaka huu, halmashauri 184 zitaanza kutumia mfumo mpya.

Aidha, lengo la kushirikisha taasisi zingine za serikali ni kujifunza jinsi mifumo hiyo ya ukusanyaji mapato itakavyokuwa ikifanyakazi ili kuwarahisishia kazi zao.



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alipofanya ziara ya kukagua athari za mvua katika Barabara ya Nyerere, eneo la Nkurumah, aliiagiza Mamlaka ya Jiji hilo, kuzibua miundombinu ya majitaka haraka ili kuondoa kero kwa wananchi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jaji Mkuu ahimiza utatuzi migogoro kwa usuluhishi

**Na Grace Gurisha**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amesema eneo la uhimizaji wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi nchini halipewi kipaumbele na wadau wa mahakama.

Prof. Juma alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu wiki na siku ya sheria nchini kwa mwaka 2023 jijini Dar es Salaam.

Alisema utafiti unaonesha nchi nyingi zilizoendelea, usuluhishi humaliza zaidi ya asilimia 90 ya migogoro inayofikishwa mahakamani.

"Hali hiyo ni tofauti na nchi yetu ambapo licha ya Ibara ya 107A (2) (d) ya Katiba ya nchi kuhimiza utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi, bado eneo hili halipewi kipaumbele na wadaawa na wadau wa mahakama kwa ujumla," alisema Prof. Juma.

Alisema hali hiyo inathibitishwa na idadi ndogo ya mashauri yanayomalizika kwa njia ya usuluhishi.

"Hali hii imeisukuma Mahakama ya Tanzania kuwa na kaulimbiu yenye lengo la kuhimiza utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi," alisema.

Pia aliwahimiza wananchi wa Mkoa wa Dodoma ambako maonesho ya wiki ya sheria kitaifa yatafanyika, wafike kwenye viwanja vya Nyerere Square ili wapate elimu mahsusi kuhusu utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi.

"Wananchi watakaofika kwenye viwanja hivyo watapata nafasi ya kutoa malalamiko, maoni na mapendekezo ya uboreshaji wa huduma za mahakama," alisema.

Alisema maadhimisho hayo ya wiki ya sheria yatafanyika kuanzia Januari 22 hadi 29 na yatafunguliwa kwa matembezi na mgeni rasmi anayetarajiwa kuwa Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango.

Aidha, kilele cha maadhimisho hayo ni Februari Mosi, katika viwanja vya Chinangali, jijini humo na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi katika kukuza uchumi endelevu, wajibu wa mahakama na wadau'.

Alisema kaulimbiu hiyo imebeba ujumbe mahususi kuhusu wajibu wa mahakama na wadau wake kutumia njia ya usuluhushi kutatua migogoro kwa lengo la kukuza uchumi endelevu.

**KABWELA** Fadhili Mohamed






Baadhi ya watumishi wa Tembo Nickel wakigawa bidhaa za chakula, afya na elimu kwenye msimu wa Krismasi, zenye thamani ya Sh. 5,325,000 kwa vituo vya Mother Theresa Rulenge, Angles Home Rulenge na Nazareth Centre Ngara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zaidi ya wanafunzi 400 wasomea chini ya miti

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI 484 wa Shule ya Msingi Butibu katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wanalazimika kusomea chini ya miti baada ya vyumba vinne vya madarasa kati ya 10 vilivyoko kuezuliwa na mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali.

Tukio hilo lilitokea Novemba 15, mwaka jana na kusababisha baadhi ya wanafunzi kukosa sehemu nzuri ya kusomea na kulazimika kusomea chini ya miti inayozunguka shuleni hapo kwa awamu.

Shule hiyo yenye jumla ya wanafunzi 1,209, kati yao wa kiume 582 na wa kike 627 huku vyumba 10 vilivyoko, vinne na ofisi ya walimu vikibomolewa na mvua hiyo na sita vikitumika na baadhi ya wanafunzi na 484 wakisomea chini ya miti.

Wakiwasilisha kilio chao kwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, wakati akikagua miradi mbalimbali ya maendeleo, kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo, baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo walisema adha hiyo imekuwa ikiwatatiza hususani wakati wa vipindi vya mvua na kuwakosesha masomo.

Colletha Katemi, mwanafunzi wa darasa la pili alisema, wanalazimika kufua kila siku kutokana na kuchafuka nguo zao kwa kukaa chini.

Alisema wakati mwingine wanashindwa kuwa makini kumsikiliza mwalimu na kuandika vyema kutokana na hali ya mazingira wanayosomea na kuiomba serikali kuwajengea madarasa mengine mapya yatakayowasaidia kujisomea kwa makini na kutimiza ndoto zao.

Alisema kuwa wanapokuwa wakisoma chini ya miti mawazo yanahama na kuanza kuangalia wapita njia na wengine kutoroka masomo hali inayomfanya mwalimu pia kutotambua mwanafunzi gani yupo na nani hayupo na kwamba kama suala hilo lisipotatuliwa kwa haraka watazidi kukosa masomo yao.

Shija Cosmas, anayesoma darasa la nne, alisema licha ya kusoma katika madarasa kwa kubanana wanalazimika kugawanywa na wengine kusomea chini ya miti hali inayowafanya kutomudu masomo wakati mwalimu akifundisha hususani somo la Hisabati na Sayansi.

Mwalimu Mkuu, Igimbi Tungu, alisema shule hiyo ilikuwa na vyumba vya madarasa 10 kati ya hivyo vinne na ofisi ya walimu vililiezuliwa na mvua iliyoambatana na upepo na vyumba sita vilivyobaki vikitumiwa na wanafunzi 1,209.

Alisema, licha ya shule awali kuwa na vyumba hivyo, walikuwa wakikabiliwa na uhaba wa vyumba vya madarasa 26 ili kufanikisha wanafunzi wote kusomea madarasani na wazazi wamechangisha fedha na kujenga maboma mawili ya vyumba vya madarasa ili kuwanusuru wanafunzi hao.

Semeni Nyambi, mzazi alisema, serikali inatakiwa kuchukua hatua za haraka kukabiliana na tatizo hilo kwa kukamilisha baadhi ya vyumba vya madarasa walivyoanzisha ujenzi kwa nguvu zao kwa kuwa kipindi hiki ni cha mvua za masika na inaponyesha inasababisha wanafunzi kukosa masomo yao.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Charles Mbulu, ambaye ni Ofisa Elimu wa Shule za Msingi alisema, halmashauri imetenga fedha za dharura Sh. milioni 60 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vinne na ofisi moja ya walimu vilivyoezuliwa na mvua na wanafunzi wataendelea kusomea chini ya miti kwa muda huku wakiendelea na ujenzi.

Mbunge wa Jimbo la Ushetu alisema, kukamilisha vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi inahitajika Sh. milioni 26 na kwasababu mifumo ya fedha imeshafunguka ni vyema halmashauri ikatoa fedha hizo na amechangia Shilingi milioni nne kutoka Mfuko wa Jimbo ili kuwasaidia wanafunzi kusoma katika mazingira rafiki.

## Othman aomba Japan kupanua wigo wa ushirikiano mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameiomba Serikali ya Japan kuangalia uwezekano wa kupanua wigo wake wa ushirikiano na Zanzibar kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi hasa katika maeneo ya fukwe zinazoharibika Unguja na Pemba.

Othman, alitoa ombi hilo, alipokutana na Balozi wa Japan nchini Tanzania, Misawa Yusushi kwa mazungumzo rasmi yanayohusu ushirikiano kati ya nchi hiyo na Tanzania ikiwamo Zanzibar.

Alisema kutokana na athari ya mabadiliko ya tabianchi inayoendelea, yapo maeneo kadhaa katika visiwa vya Unguja na Pemba, yakiwamo ya kilimo na mkaazi ya watu kama vile Nungwi, Jambiani na Tovuni, maji ya bahari yanaendelea kusogea na kuleta athari kwa jamii.

Kadhalika, alisema suala la mabadiliko ya tabianchi limesababisha athari kubwa ya kimazingira na kuonekana kuwa ni tishio kubwa kwa wananchi wa Zanzibar hasa maeneo ya makazi ya watu yanapovamiwa na maji ya chumvi na kuathiri shughuli nyingine za kijamii na kilimo.

Alisema pamoja na jitihada za serikali za kukabiliana na hali hiyo kupitia uhifadhi wa mazingira, suala hilo linahitaji uwezo mkubwa wa kiufundi, kitaalamu na kifedha katika kukabiliana nalo na ni vyema serikali ikaangalia maeneo zaidi katika kuisaidia Zanzibar.

Aliyataja maeneo mengine yaliyo chini ya ofisi yake ambayo ni muhimu kuwapo na kuzidisha wigo wa ushirikiano wa namna hiyo ni pamoja na suala la mazingira, mapambano dhidi ya dawa za kulevya na masuala ya udhalilishaji.

Alisema Zanzibar inathamini na kuridhishwa na ushirikiano kati yake na Japan kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo sekta ya uchumi wa buluu na uvuvi inayotekelezwa kwa pamoja na serikali na nchi hiyo.

Balozi wa Japan, alisema nchi yake ina ushirikiano wa muda mrefu na Tanzania ikiwamo Zanzibar na itaendelea na jitihada hizo ili kuisaidia Zanzibar katika maeneo tofauti.

Alisema Zanzibar ina fursa nyingi za ushirikiano na Japan na itaendelea kuangalia maeneo zaidi katika kuendeleza ushirikiano huo kwa kuwa nchi yake pia ni ya visiwa kama Zanzibar.





## Polisi wapewa onyo kujihusisha, kushabikia siasa

**Na Cynthia Mwilolezi** ARUSHA

ASKARI wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha wameonywa kutojihusisha na ushabiki wa vyama vya siasa badala yake wajikite katika ulinzi wa raia na mali zao.

Onyo hilo lilitolewa na Kamanda wa Jeshi la Polisi wa Kikosi cha Kuzuia Wizi wa Mifugo nchini, Kamishina Msaidizi wa Polisi (ACP), Simon Pasua, wakati wa hafla ya kuwapongeza askari walio fanya vizuri zaidi mwaka jana mkoani Arusha.

Kamanda Pasua alisema kuwa askari wanapaswa kushabikia masuala mengine ya kijamiii kama vile michezo na kujikita zaidi katika ulinzi wa raia na mali zao ili kuleta ufanisi na kupunguza manung'uniko ya wananchi.

"Naonya askari acheni kujihusisha na masuala ya siasa kaeni mbali na nyie kazi yenu kuhakikisha mnaimarisha ulinzi na usalama kwa ajili ya mali za wananchi na nyumba zao," alisema.

Kuhusu askari waliopewa zawadi alisema wana muda wa kuongeza juhudi ili mwaka mwingine waendelee kupata zawadi hizo ikiwa ni pamoja na kupanda vyeo.

Hivyo, aliwataka kufanya kazi kwa umoja ili kuleta ufanisi wa kazi za Jeshi la Polisi nchini na wananchi.

Katika hafla hiyo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alimpongeza Kamanda wa kikosi hicho kwa kutambua mchango wa askari wanaofanya kazi vizuri.

"Watanzania wanalitegemea sana Jeshi hili, nyie mliofanya vizuri kwenye Jeshi hili mtaliwakilisha vyema Jeshi na kutafuta wengine kuiga mfano wenu ili nao wapate zawadi kipindi kingine," alisema.

Baada ya onyo hilo askari wa kikosi hicho kutoka makao makuu ya kikosi cha kupambana na kuzuia wizi wa mifugo, Koplo, Silvester Mang'aha, aliyepata zawadi kwa kufanya kazi vizuri mwaka 2022, aliwashukuru askari wenzake kwa kumpa ushirikiano.

# Lugha ya kiarabu kuanza kufundishwa vyuo vikuu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, amesema serikali inafikiria kuongeza lugha ya kiarabu katika orodha ya lugha za kimataifa zitakazofundishwa nchini kupitia vyuo vya kati na vyuo vya elimu ya juu.

Aidha, amesema mchakato wa mapitio ya sera na mitaala mipya ya elimu iliyokuwa ikihakikiwa umekamilika na kwamba baada ya kushirikisha wadau mbalimbali, sasa upo tayari kwa mjadala wa kitaifa kuhusu mapendekezo ya sera ya elimu na mitaala.

Prof. Mkenda aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wakuu wa vyuo vya elimu, maofisa elimu na wakufunzi na wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Marangu kilichoko Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

"Wizara imefanya kazi kubwa katika mchakato mzima wa kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, ambapo kwa sasa mchakato wa ndani ya Wizara umekamilika na kinachosubiriwa ni mchakato wa ndani ya serikali, kabla ya kuandaa kongamano maalumu la kitaifa la kukusanya maoni ya wananchi.

"Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Ualimu Marangu, kaa na wajumbe wako na mjadili na kupendekeza kuongeza lugha ya kiarabu katika lugha zitakazofundishwa kuanzia sasa," alisema.

Katika mapitio hayo ya sera na mitaala, Waziri Mkenda, alisema serikali imezingatia ujenzi, mapitio na maboresho ya vyuo vyote vya ualimu kwa kuwa ndiyo mboni au jicho la elimu nchini.

Waziri Mkenda alisema kwa sasa kwa kuwa kuna vyuo 35 vya serikali na vyuo vingine vya taasisi na vya binafsi, kuna kila sababu ya kuvitazama kwa umakini ili kuboresha sekta ya elimu nchini.

Alisisitiza kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, itaimarisha uboreshaji wa vyuo vya ualimu, ikiwamo miundombinu na upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia ili kuimarisha sekta ya elimu nchini.

Pia, Waziri Mkenda alisema kuwa serikali itaweka mkakati mzuri wa elimu ili kusaidia walimu nchini kuweza kujiendeleza pamoja na kuongeza ujuzi.

Katika ziara yake, Prof. Mkenda, alisisitiza kuwa ndoto ya serikali ni kuona mwalimu anajiendeleza ili aweze kuwa bora hivyo msimamo wa serikali ni kuwaruhusu walimu kujiendeleza ndani na nje ya nchi.

Oktoba 9, mwaka jana katika kilele cha Siku ya Walimu Duniani iliyofanyika katika Wilaya ya Bukombe, mkoani Geita, Waziri Mkenda alinukuliwa akisema: "Mwalimu akiomba ruhusa ya kwenda kusoma mpe ruhusa, mwalimu ni ufunguo wa maisha katika maendeleo ya nchi yetu, mafunzo kazini yataendelea, Serikali imetenga bajeti kwa ajili ya kuwaendeleza".



Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Hanang', mkoani Manyara, Thomas Akonaay (kulia), akiwa amekaa kwenye moja ya viti na meza vya Shule ya Sekondari Mulbadaw, wakati kamati ya siasa ya CCM wilaya hiyo, ilipotembelea miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani humo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Watu wenye ulemavu 1,296 wapata msamaha wa matibabu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imesema idadi ya watu wenye ulemavu waliopata msamaha wa matibabu katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro kwa mwaka jana wamefikia 1,296.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Halmashauri hiyo, Dk. Alex Kazura, wanufaika wa mpango huo walipata huduma hiyo katika zahanati na vituo vya afya 54 vinavyomilikiwa na serikali.

Dk. Kazura alikuwa akitoa taarifa ya mrejesho kwa wajumbe wa Jukwaa la Wanawake na Wasichana Wenye Ulemavu, Mkoa wa Kilimanjaro, waliokutana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Kastori Msigala na kufanya nae mazungumzo kuhusu utekelezaji wa mpango huo.

"Watu wengi wenye ulemavu tunawatibu kwa njia ya msamaha na katika vituo vyetu vya afya na zahanati zetu 54 vinavyomilikiwa na serikali. Kwa mwezi karibu kila kituo kinaweza kikapata wateja wawili, ambao wanafika kituoni kutibiwa kwa mfumo wa msamaha.

"Ukiangalia 54 mara mbili ni wastani wa watu 108 kwa mwezi na ukiifanya kwa miezi 12, inakupa picha halisi ya mwaka, kwa idadi ya watu wanaopata huduma za afya kwa njia ya msamaha katika halmashauri yetu ni 1,296."

Mwenyekiti wa jukwaa hilo, Linda Macha, alisema katika ufuatiliaji wao walitaka kujua idadi ya watu wenye ulemavu wanaopata huduma ya afya bure pamoja na utoaji wa huduma ya afya kama mazingira yako rafiki.

Aidha, alisema pia jukwaa hilo lilitaka kujua vitanda vilivyopo kwenye maeneo ya kutolea huduma za afya kama hospitali, vituo vya afya na zahanati ni rafiki kwa watu wenye ulemavu wa aina zote.

Alisema kazi ya jukwaa hilo ni kufanya utetezi na ushawishi kwa watu wenye ulemavu Kilimanjaro.

Alisema: "Tumekutana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, kupata taarifa juu ya huduma za afya kwa jamii ya watu wenye ulemavu kwa sababu kila mtu ni haki yake na ana stahili kujua afya yake.

"Tulichotaka kujua ni idadi ya watu wenye ulemavu wanaopata huduma ya afya bure na utoaji wa huduma ya afya katika zile sekta zake kama mazingira yako rafiki kwa watu wenye ulemavu".



# H'shauri yajenga shule tano kukabili ongezeko wanafunzi

**Na Ndalike Sonda,** MEATU

HALMASHAURI ya Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu imejenga shule mpya tano za sekondari kwenye kata ambazo hazikuwa na shule.

Pia imewapeleka walimu 20 katika shule hizo ili kuwaondolea wanafunzi adha ya kutembea umbali mrefu kufuata masomo katika kata jirani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Msoleni Dakawa akizungumza na waandishi wa habari alisema tayari imewapeleka walimu 20 kwenda kufundisha katika shule hizo.

Dakawa aliwataka walimu hao kwenda kutimiza wajibu wao kwa kuwa serikali imewekeza fedha nyingi katika kuboresha miundombinu.

Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari Wilaya ya Meatu, Hadija Rajabu aliwasihi walimu kuwa walezi wazuri wa wanafunzi ili kuongeza uelewa wa masomo na kuwa na ufaulu mzuri katika masomo yao.

"Watumishi wenzangu pamoja na kuwa ninyi ni walimu, pia ni walezi nendeni mkawe walezi wa wanafunzi kama wazazi ili wanafunzi waelewe masomo mtakayowafundisha na lazima kwanza muwapende na kuwajali, Serikali inawategemea sana katika kuleta matokeo chanya kweye sekta ya elimu,"alisema Rajabu.

**Shule hizo mpya zilizofunguliwa na masomo kuanza Janauri juzi ni pamoja na Shule ya Sekondari Mwananimba, Isengwa, Masalinge , Busangwa na Mwashagata.**

Mkuu wa Divisheni Utumishi, Utawala na Rasilimali Watu Wilaya ya Meatu, Rashidi Semgoya aliwahakikishia walimu waliopelekwa katika shule hizo watapewa stahiki zao kwa wakati na kuwataka wazingatie sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya serikali katika kutekeleza majukumu yao.

Shule hizo mpya zilizofunguliwa na masomo kuanza Janauri juzi ni pamoja na Shule ya Sekondari Mwananimba, Isengwa, Masalinge , Busangwa na Mwashagata.



Kijana Yusuph Hamis 'Mr Phone', aliyejiajiri katika shughuli za ufundi simu kwa zaidi ya miaka 15, akiwa kazini ofisini kwake katika Manispaa ya Shinyanga jana. Kijana huyo, alisema kuwa kazi hiyo inamsaidia kujiingizia kipato na kujikimu kimaisha na kuwataka vijana wenzake kujenga tabia ya kujiajiri na kuacha kukaa vijiweni. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mila, desturi kandamizi kikwazo mapambano kutokomeza ukatili

**Marco Maduhu,** SHINYANGA

JAMII kuendelea kukumbatia mila na desturi kandamizi imetajwa kuwa ni chanzo cha kuendelea kushamiri kwa matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani Shinyanga, Aisha Omary, alibainisha hayo jana kwenye Jukwaa la Wanawake wilayani humo lililofanyika katika Kata ya Iselamagazi.

Alisema serikali wilayani humo imekuwa ikijitahidi kutoa elimu kwa wananchi juu ya madhara ya vitendo vya ukatili wa kijinsia, ikiwamo na kuwaozesha watoto wadogo, lakini tatizo ambalo linasababisha matukio hayo kuendelea ni jamii kukumbatia mila na desturi kandamizi.

"Jamii ikiachana na kukumbatia mila na desturi kandamizi, ukatili wa kijinsia hautakuwapo kabisa wala kusikia mtoto ameozeshwa ndoa ya utotoni,"alisema Omary.

Baadhi ya wanawake wilayani Shinyanga akiwamo, Suzana John ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Ibubu, alisema vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia ili vipate kukoma ni lazima wanaume wapewe elimu kwa kina kuachana na mila kandamizi ambazo husababisha mfumo dume.

Mkurugenzi wa Shirika la Young Women Leadership, Beatrice John, aliwataka wanawake na viongozi wa jukwaa hilo waendelee kupaza sauti juu ya vitendo vya ukatili wa kijinsia, ili wahusika wachukuliwe hatua.

# KACU yatenga milioni 949/- ujenzi ofisi ya kisasa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

CHAMA Kikuu Cha Ushirika Kahama (KACU) mkoani Shinyanga, kimetenga Sh. milioni 949.96 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya kisasa ya chama hicho.

Fedha hizo zimetokana na makusanyo ya mapato ya ndani kupitia ushuru wa tumbaku.

Mwenyekiti wa chama hicho, Hamisi Majogoro, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kusema kuwa ofisi hiyo itakuwa na ukumbi wa mikutano ambao utakuwa na uwezo wa kuingiza watu 500.

Alisema mapato yanayotarajiwa kupatikana yatatokana na malipo ya ushuru wa tumbaku kwa kuzalisha kilo milioni 16.860 kwa msimu wa uzalishaji wa mwaka 2022/2023, kwamba ushuru wake utakuwa ni Sh. bilioni 1.173 kati ya hizo Sh. milioni 949.96 zitatumika katika ujenzi wa ofisi ya chama.

Majogoro alisema makusanyo hayo yatakusanywa kwa misimu mitatu kuanzia mwaka 2022 hadi 2025 na kila mwaka watakuwa wakikusanya ushuru wa Sh.bilioni 1.173.

"Majengo tunayotumia sasa ni ya zamani sana na yako mbalimbali na inatuwia vigumu kuwasiliana katika utendaji kazi wetu, hivyo tumeamua kutenga fedha kupitia ushuru wa tumbaku ambao tutakusanya ili tujenge ofisi ya kisasa ya ghorofa moja ambayo itakuwa na ukumbi wa kubeba watu 500,"alisema Majogoro.

Hata hivyo aliwataka wakulima kila mmoja kuhakikisha wanazalisha kilo za tumbaku kulingana na mikataba waliyoingia na kampuni za ununuzi wa zao hilo ili kufikia lengo la uzalishaji wa kilo milioni 16.

Alisema hali hiyo itawawezesha kukusanya ushuru ipasavyo na kutenga fedha za ujenzi na kuondokana kutumia majengo ya zamani.

Mmoja wa wakulima kutoka Ushetu-Bukomela, Kulwa Shoto alisema ili kufikia lengo ya kilo hizo ni vema wakapata pembejeo za kilimo hususani za kukuzia kwa wakati na kuhakikisha wanatembelewa na maofisa ugani na kuwapatia elimu na kuhakikisha wanapata tumbaku bora.

Pia aliomba kuondolewa kwa ushuru wa asilimia tano kwa kila kilo moja inayotozwa na Halmashauri ya Ushetu ambayo inatumika kulipa gharama za magongo yanayotumia kukaushia zao hilo, kwamba wamekuwa wakitumia gharama kubwa katika uzalishaji ila mapato wanapata kidogo.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, aliyekuwa Mwenyekiti wa KACU alisema, suala la kuondoa asilimia tano ya ushuru wa kuni za kuchomea tumbaku atahakikisha linaondolewa, kwamba atashirikiana na KACU.

Alisema wakati wa mavuno na uchomaji wa tumbaku watahakikisha wanafuata kanuni bora za kilimo na kupata tumbaku yenye ubora unaohitajika katika masomo ya kimataifa, kwamba hali hiyo inafanya KACU kupata ushuru wake ipasavyo na halmashauri kupata mapato ya kutosha.

Vyama vinapochekelea uhuru mikutano, vianze na kutii angalizo
Ukurasa 12



Ukurasa 14



Taliban kundi kandamizaji kwa wanawake, wasichana

siasa
JUMATANO JANUARI 11, 2023
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

UJIO MIKUTANO

# Vyama visiwe muuaji maendeleo demokrasia

**Na Mwandishi Wetu**

VYAMA vya siasa vimerejeshewa uhuru wa kufanya mikutano ya hadhara na kukutana na wanachama na wananchi bila kukwazwa wala kuvurugwa na mkono wa dola.

Hata hivyo, baadhi ya vyama vya siasa licha ya kulilia kuwapo kwa uhuru huo na mikutano ni wakati wa kuzitafakari njia zake.

Visiishi kwa kukariri viache kuwa ukanda wa unyanyasaji wa wanachama na raia, kukiuka haki za binadamu, uongozi usio na nidhamu usiojali sheria na kujiamulia mambo kama wakubwa au viongozi wake wanavyopenda.

Vyama vya siasa baada ya kuwekewa zuio la mikusanyiko na mikutano ya ndani na nje kwa miaka saba sasa, vilipiga kelele kulalamika nje na ndani ya mipaka vikitaka kufunguliwa na kuendeleza michakato ya kidemokrasia kupitia hadhara.

Vyenyewe vililaumu kufungiwa na kuhusisha hali hiyo na uongozi usiojali demokrasia, sheria wala katiba, utawala wa kiimla na kwa ujumla kuilaumu zaidi awamu ya tano.

Lakini, ukweli ni kwamba kuna baadhi licha ya kulalamikia kubinywa uhuru na demokrasia ya vyama vingi, ndani ya taasisi hizo ni kama ndege zinazorushwa na marubani wasio na mafunzo ya urubani.

Uongozi wa baadhi ya vyama unadaiwa si wa kuridhisha viongozi wanalalamikiwa. Wako wenyeviti waliodumu kwa miongo mitatu sasa. Ndani ya baadhi ya vyama ni ugomvi na utawala wa kimabavu unajiri, kuna kujuana kwingi na ukiukaji wa haki za binadamu unaotokana na 'siasa za kidikteta' unaoonekana kwenye masuala ya kimaslahi.

Licha ya vyama hivyo kudai demokrasia, vipo vingi ambavyo havina demokrasia. Hakuna kuandaa viongozi



John Cheyo, Mwenyekiti wa UDP tangu 1992. **PICHA: IPP MEDIA**

wala kurithishana majukumu.

Vimekuwa ni uwanja wa migogoro na kusababisha wanachama kuhama huku jamaa au waasisi wa vyama wakiishi madarakani kwa muda wote.

Vyama vya siasa japo si vyote vimejaa 'madikteta,' ukandamizaji na uongozi wa kiimla usiokuwa na demokrasia na hii inaonekana kwenye migogoro inayoibuka ndani yake hadi wanachama wanasambaratika.

Lakini mambo hayaishii hapo kunaibuka tena migogoro ndani ya baadhi ya vyama ambavyo unawalazimisha wanachama kuhama na kuachana na taasisi waliyoiasisi kwa na kuitumika kwa miaka mingi.

Aidha, mgawanyiko huo unaendelea kwa kuwasimamisha uanachama viongozi kadhaa na wanachama kwa tuhuma ambazo ukizifuatilia pengine ni kuwa na mawazo yanayopingana na uongozi wa kimabavu.

Vyama hivyo vimekuwa kwenye migogoro kwa miaka bila kupata ufumbuzi si wa mahakama wala Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

Ipo migogoro ya kiuongozi iliyoshuhudiwa hivi karibuni ya kufanyika mapinduzi na kumng'oa mwenyekiti wake ambaye naye ana miongo mingi kwenye wadhifa huo.

Kadhalika baadhi ya vyama vikongwe vimo kwenye kapu la uongozi wa kudumu na usiokubali mawazo mbadala, hivyo wakati wanahamasisha kupewa haki ya jumuiko na kuzungumza na wanachama vijitafakari vinafanya nini kuhamasisha utawala bora, demokrasia na shughuli nyingine za kimaendeleo ndani ya vyama vyao.

**KATIBA VYAMANI**

Wakati mwingine ni vyema kusikia sauti nyingi zikidai katiba mpya na bora, uchaguzi huru na haki, lakini ndani ya vyama vya siasa kuna mikakati kuwa na katiba mpya zenye kueleza namna ya kuuwajibisha uongozi wa chama?

Katiba zenye mipango ya kuinua na kuwahirikisha wanawake na vijana kwenye miradi na kazi za kidemokrasia? Vipi kuhusu kusimamia na kutumia fedha na rasilimali za chama kuendeleza demokrasia, uchaguzi wa haki, utawala bora na kuleta maendeleo?

Ukweli ni kwamba vipo vyama vya siasa ambavyo pia vinavunja katiba, vinakiuka haki za binadamu na kukumbatia mambo ambayo hayawafurahishi wanachama wake.

Vyama vya siasa ni kama mbwa walinzi wanaopaswa kusimamia utawala bora, uongozi kwa misingi ya sheria na katiba, demokrasia pamoja na kuheshimu haki za binadamu, ushirikishwaji wanawake, vijana, watu wenye mahitaji maalumu na matumizi bora ya rasilimali za umma.

Ndani ya vyama vya siasa kunafanyika uteuzi usiolalamikiwa wa washiriki wa uchaguzi? Uchaguzi huo unakuwa huru, wa haki na wa uwazi unaoruhusu wanachama kukataa matokeo na hata kuyapinga mahakamani?

Kama ni suala linalohusu demokrasia, utawala bora, uchaguzi ulio huru na haki, katiba, haki za binadamu na wanachama mhusika namba moja ni mwanasiasa ambaye ni zao la chama cha siasa.

Kwa hiyo kuanzia CCM, ACT-Wazalendo, CHADEMA, NCCR-Mageuzi, CUF, ADC, UDP, TLP wote wanahusika na ukweli ni kwamba ni jukumu lao bila kujali viko madarakani au ni vya upinzani.


Vyama vya siasa vising'ang'anie kuwa na uhuru wa kukutana na kufanya mikutano ya hadhara bali pia vikumbuke kazi muhimu ya jukumu la kuandaa viongozi na watawala wanaoongoza na watakaoliongoza taifa kuanzia madiwani, wabunge na mawaziri bora.

Kwa vile kwa mujibu wa katiba ya Tanzania, yeyote anayeongoza kwenye siasa kuanzia diwani, mbunge, waziri, rais au waziri mkuu ni lazima apitie kwenye mchakato wa chama cha siasa, hivyo viwe na katiba zinazoainisha demokrasia za kuandaa viongozi siyo kusalia madarakani kwa miongo yote na kugawana madaraka kwa misingi ya udugu na urafiki.

**WAPI DEMOKRASIA**

Ukweli uliopo ndani ya baadhi ya vyama vya siasa ni kwamba maeneo haya au viwanda vya kuzalisha wanasiasa, kama wabunge, mawaziri, marais na madiwani ambao ni muhimu kwenye kujenga na kuimarisha demokrasia hayana

INAENDELEA UK. 12



Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya mkutano na viongozi Abdulrahman Kinana-CCM na Freeman Mbowe (kushoto) wa CHADEMA hivi karibuni. **PICHA:IKULU**

# Vyama vinapochekelea uhuru mikutano, vianze na kutii angalizo

**Na Ani Jozeni**

MAZINGIRA mapya ya kisiasa yanaibuka Tanzania, katika hali ambayo kwa kiasi fulani ni kama kuanza upya kwa mfumo wa vyama vingi .

Upya huo haumaanishi pambazuko jpya kwani washiriki wa siasa ni wale wale licha ya kuwa kila chama cha siasa kitakuwa na wachache walioondoka ikiwa ni pamoja na kustaafu shughuli za kila siku, hivyo nyuso mpya zipo pia.

Suala lipo katika mazoea yaliyoanza kuota mizizi kwa miaka takriban saba; si kipindi kifupi maana ni karibu muongo mmoja.

Unaweza kuona hali hiyo katika baadhi ya mijadala inayoibuka kuhusu mfumo wa vyama vingi, kuwepo kwa mikutano ya hadhara, na wengine kuamini kuwa sasa taifa limeanza pia mchakato wa kufikia katiba mpya.

Inakuwa kana kwamba masuala hayo yameunganishwa, na hata katika maelezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, ni kama yaliendana ila kuna angalizo la usikivu.

Suala la kuanza tena hadhara za kisiasa liliambatana na tahadhari za kufanya siasa tulivu zinazoendana na utamaduni wa kijamii na kwa maana hiyo kisiasa; kuwepo na adabu pamoja na heshima.

Suala la katiba mpya halikuwa katika mtiririko unaohusu kurudishwa kwa mikutano ya hadhara ila kama hatua nyingine ya maridhiano ya kisiasa yanayoendelea.

Unaweza kusema pia kuwa licha ya kuwa Rais Samia hakusema hivyo waziwazi kuwa ajenda inayofuata katika suala la maridhiano, yaani kuangalia upya sheria kama ile ya vyama vya siasa au sheria ya uchaguzi (bila kuingiza hapo sheria ya jeshi la polisi) itategemea kufaulu kwa hatua ya kwanza ya maridhiano.

> Ni suala la kisaikolojia kuwa mwelekeo huo unaona jambo ambalo pia alilitaja Rais Samia, anakiri kuwa mikutano ya hadhara ni haki ya kikatiba, iliyozuiliwa kimakosa kwa muda mrefu.

Ni jukumu la vyama vya siasa kufanya siasa za kistaarabu, kuwezesha hatua nyingine za maridhiano zifuate, katika mwendelezo wa utulivu.

Kuunganisha kihisia kurudishwa kwa mikutano ya hadhara na kuendelea na mchakato wa katiba mpya, kuwa ni jambo moja au lenye pande mbili tofauti, ni mtazamo kuhitaji kutafakari upya kilichozungumzwa katika hotuba ya kutoa ruhusa hiyo.

***Ni suala la kisaikolojia kuwa mwelekeo huo unaona jambo ambalo pia alilitaja Rais Samia, anakiri kuwa mikutano ya hadhara ni haki ya kikatiba, iliyozuiliwa kimakosa kwa muda mrefu.

Rais anatoa angalizo kwa la nini kifanyike katika mikutano hiyo na nini kisifanyike. Kwa maana nyingine rukhsa ya Rais Samia iko ila vyama vya siasa vihakikishe kuwa vianzio vya kuzuia mikutano hiyo havijitokezi tena, na hasa siasa vurugu, kuhamasisha fujo na kuhoji uhalali wa serikali iliyoko madarakani.

Kwa lugha nyingine, kuruhusu mikutano kama haki ya kikatiba kusingefuatana na tahadhari zozote, kwani katika nchi za kidemokrasia vyama havielekezwi na serikali nini kifanyike katika mikutano ya hadhara na kiishie wapi.

Ina maana kuwa maridhiano yanakubalika au yamekubalika katika ngazi za juu cha chama tawala kwa sharti la kuwa na mikutano inayoheshimu mamlaka.

Ukiangalia ruhusa hiyo ya kufanya mikutano ya vyama vya siasa kwa sharti kuwa hawatafanya mikusanyiko inayolenga kuhatarisha amani na utulivu nchini, halafu uongezee matazamio ya mabadiliko ya kikatiba.

Kuna dhana ya utamaduni wa kisiasa, ambayo imetoa ruksa ya mikutano ya kisiasa na hoja nyingine ya pili ya kujivua gamba na kusisitiza umoja wa kitaifa kutambua uhuru wa kisiasa bila kupingwa.

Ni jambo la wazi kuwa wapo wanasiasa wenye ushawishi mkubwa miongoni mwa wasomi na mabalozi wa nje walioko nchini. Ila wafuasi wao ambao hawaelewi masuala ya utamaduni wa kisiasa na sharti la umoja na utulivu si wengi, ndiyo maana uhuru wa kufanya mikutano uliondolewa kwa miaka saba na hakuna chama kilichofaulu kuitisha maandamano kupinga hali hiyo.

Ina maana kwamba vyama vya siasa vitumie uhuru huo kwa uangalifu, ili kuwepo na mabadiliko ya kikatiba na kuweka mazingira ya kuzitazama upya sheria, kuimarisha umoja wa kitaifa kama Rais Samia anavyosema kuwa mbadiliko mengine yataendelea hatua kwa hatua.

# Vyama visiwe muuaji maendeleo demokrasia

INATOKA UK. 11

'demokrasia'.

Hivyo vyama viache udikteta na ubabe visiongozwe kidikteta, ndiyo maana wananchi wanaweza kuwa na hofu kuwa wanasiasa hawa wanaogombana kila leo watawaongozaje wakati wenyewe hawana demokrasia, hawaelewani, wanafukuzana kila leo kutakuwa na lipi jipya?

Wanasiasa wanahitaji kubadilisha mitizamo kutoka kwenye fikra zao za kidikteta au kujipendelea ili wawe viongozi waliobadilika na kuboresha siasa, uongozi na mitizamo chanya.

**KUBORESHA VYAMA**

Ni vyema wadau kama UNDP wakasaidia kuanzisha programu maalumu ya kuimarisha demokrasia ndani ya vyama vya siasa ili kuwaandaa wanasiasa wenye mitizamo ya kidemokrasia, haki za binadamu, utawala wa sheria na wanaoheshimu katiba na uhuru wa mawazo ya kila raia.

Suala hilo litafanikisha kuvifunda vyama vya siasa na kuviwezesha kuwa na demokrasia ya kuongeza usawa kijinsia, ushirikishwaji wa vijana na makundi ya wanyonge kwa imani kwamba mpango huo utaleta matokeo makubwa kwa wananchi na taifa.

M23 WANG'ATA, KUPULIZA

# Ni kuachia makambi, lakini kushambulia, kuteka miji, vijiji




Walinda amani wa UN –MONUSCO, wakipiga doria kukabili wapiganaji wa M23, eneo la Rangira- Kivu Kaskazini, Machi 2022. **PICHA: REUTERS.**

**Na Christina Mwakangale**

JUMATANO iliyopita Januari 5, ilikuwa siku ya kundi la waasi la M23 la nchini DRC, kuondoka kwenye kambi ya kijeshi ambayo liliinyakua Oktoba, mwaka jana kutoka kwenye majeshi ya serikali.

Ahadi ya kundi hilo kuachia kambi hiyo ya kijeshi iliyopo eneo la Rumangabo, mashariki mwa DRC imetimia huku baadhi ya viongozi kwenye mji wa Kibumba, wakiripoti waasi hao wameanza kuondoka na shughuli zikianza kurejea katika hali ya kawaida.

Katika taarifa yake, kundi hilo lingekabidhi kambi ya Rumangabo, Alhamisi iliyopita, kwa wanajeshi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ikiwa ni hatua iliyotokana na makubaliano yaliyofikiwa mwaka jana, jijini Luanda nchini Angola.

Mvutano wa pande tatu kati ya nchi ya Rwanda na DRC na ule wa waasi wa M23, ulijitokeza kwa mara ya kwanza mwaka 2012 lilipouteka kwa muda mji wa Goma, kabla ya kufurumushwa,

Kundi hilo likaibuka tena mwishoni mwa 2021 na kuanzisha mapambano mapya, kwa madai kwamba DRC ilishindwa kutimiza ahadi yake ya kuwajumuisha kwenye jeshi, miongoni mwa malalamiko mengine mengi.

Hata hivyo, ahadi ya waasi hao kuondoka tayari imeanza kuonekana, wiki iliyopita Serikali ya Uganda, imepeleka wanajeshi wake katika eneo la mpaka wa nchi hiyo na DRC katika wilaya ya Kanungu, ambako waasi wa M23 wanaingia katika mji wa Ishasha, baada ya kuondoka Kibumba.

Kwa mujibu wa Luteni Kanali Robert Nahamya wa Jeshi la Uganda, wanajeshi hao wa Uganda, walitumwa kwenda tangu Alhamisi ya wiki iliyopita, lengo ni kutoa usalama kwa raia wake wanaoishi mpakani na eneo lenye uasi. Kadhalika Kenya, Januari 6, mwaka huu, wanajeshi wake wameripotiwa kuwasili katika kambi kubwa ya kijeshi ya Rumangabo, ambayo ilikuwa inashikiliwa na waasi wa M23.

Vikosi hivyo ni sehemu ya vikosi vya Jumuiya ya Afrika Mashariki nchini DRC.

Kuwasili kwa wanajeshi hao, ni sehemu ya makubaliano yaliyofikiwa mapema mwezi huu, baada ya waasi kuahidi kuondoka kwenye maeneo ya Rumangabo na Kishishe mkoani Kivu Kaskazini.

> Taarifa kutoka DRC zinasema, wameendelea kuchukua vijiji muhimu na maeneo ya masoko karibu kilometa 20 na mpaka wa mji wa Ishasha.

**AHADI TOFAUTI**

Wakati hayo yakiendelea, ripoti zinasema M23 wameendelea kusonga mbele katika wilaya ya Rutshuru na kuchukua eneo la Nyamilima.

Taarifa kutoka DRC zinasema, wameendelea kuchukua vijiji muhimu na maeneo ya masoko karibu kilometa 20 na mpaka wa mji wa Ishasha.

Kwa mujibu wa jeshi la DRC na ripoti za usalama za Umoja wa Mataifa, waasi wa M23 wameendelea kutuma ujumbe unaokinzana na kauli zao za wiki iliyopita, kuwa wataondoka bila masharti katika miji waliyokuwa wanaishikilia.

Hata hivyo, licha ya agizo la vikosi vya EAC, kutaka waasi hao kuachia miji wanayoshikilia chini ya makubaliano ya Nairobi na Luanda, wapiganaji hao, wameripotiwa kushambulia raia kila wanakopita.

Mapigano kati ya Jeshi la Serikali ya DRC na waasi wa M23, yalizuka Machi mwaka jana na kulazimisha watu zaidi ya 70,000 kukimbilia nchini Uganda, kuomba hifadhi, huku Rwanda ikituhumiwa kuwasaidia waasi hao.

Nchini DRC, katika mkoa wa Kivu Kaskazini, kundi la waasi la M23 linashikia mji wa mpaka wa Bunagana tangu Juni 2022. Kurejea kwa uasi huo, ulioshindwa mwaka 2013, kulisababisha watu wengi kuyahama makazi yao.

**ATHARI MGOGORO**

Umoja wa Mataifa, mashirika yasiyo ya kiserikali ya kimataifa na mamlaka mbalimbali mwaka jana, walitangaza kwamba wanahitaji karibu dola bilioni mbili, ili kukabiliana na uhaba wa chakula unaotokana na umaskini, machafuko ya kivita na uasi mashariki mwa DRC, yakitajwa magonjwa ya milipuko na utapiamlo.

Pia, watu milioni 27 au robo ya wakazi wake wanaishi katika hali hiyo. DRC ndiyo nchi yenye idadi kubwa zaidi ya watu wanaoishi katika uhaba wa chakula duniani.

Kadhalika, DRC ni kati ya mataifa ambayo ina idadi kubwa ya wakimbizi wa ndani, huku UN ikisema, zaidi ya watu 5,000,000 wameyakimbia makazi yao.

Hakuna vita kati ya Rwanda na DRC, ila kuna vita kati ya waasi hao na DRC, na Rwanda anaingia kama mtuhumiwa anayefadhili shughuli za M23.

Hicho kikiwa ndicho kiini cha uhasama wa nchi hizo, ambao pia ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

DRC haijawahi kupumzika kupambana na makundi ya waasi, tangu kuingia madarakani Rais Félix Tshisekedi, Januari mwaka 2019.

Kati ya ahadi za Rais Tshisekedi, akiingia madarakani ni kutokomeza uasi mashariki mwa nchi yake.

Jitihada za kutimiza ahadi zake ni mafanikio madogo yanayoonekana kutokana na waasi wakiwamo M23 kuwa na nguvu za kushambulia raia na wanajeshi wa DRC. Ndani ya mwaka mmoja pekee, yaani 2021; majaribio kadhaa ya kuipatanisha DRC na Rwanda, yalifanyika, huku Mei, yakifanyika mazungumzo kwa njia ya simu kati ya Rais Paul Kagame na Tshisekedi, yaliyosimamiwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU), Macky Sall.

Aidha, Juni 2021, wakuu wa EAC, walikutana jijini Nairobi Kenya, huku ajenda ikiwa ni kujadili waasi wa DRC wakati mwezi uliofuata Paul Kagame na mwenzake Tshisekedi, walikutana kwa mazungumzo ya upatanishi, yaliyosimamiwa na Rais wa Angola, Joao Laurenco. Lengo kuu, kuleta maelewano kati ya mataifa hayo.

Pamoja na mafanikio kutokuwa makubwa kama ilivyotarajiwa kutokana na ahadi za kiongozi huyo, anaonekana kufanikiwa kulishambulia kundi la M23, ama kwa kutumia mazungumzo ya kisiasa na likakubali kuweka silaha chini lakini pia kwa kutumia nguvu za kijeshi na shinikizo kutoka viongozi wa kikanda na jumuiya za kimataifa.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa na kiusalama wanaona kuwa nafasi ya jumuiya iwe ya kikanda Afrika Mshariki, Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa kuleta mtangamano, sio kuandaa vikao vya mara kwa mara kuwazungumzisha marais Kagame na Tshisekedi, bali ni kumaliza uasi na vita DRC.

***MITANDAO***

# Taliban kundi kandamizaji kwa wanawake, wasichana

## •Ni marufuku kutoka nje kusoma, kufanyakazi

**Na Maulid Mmbaga**

NCHINI Afghanistan kuzaliwa mwanamke ni shida. Ni kwa vile pamoja na ukandamizwaji wa kijinsia, kuanzia sasa huruhusiwi kuingia darasani kusoma ikiwa ni pamoja na kukatazwa kwenda vyuo vikuu lakini pia ni marufuku kufanyakazi.

Wanawake wanatakiwa kukaa nyumbani, hayo yakijiri chini ya amri zinazotolewa kwenye taifa linaloongozwa na Mawlawi Hibatullah Akhundzada, ambaye ni kiongozi wa kisiasa na kidini akiwa Kamanda Mkuu wa tatu wa kundi la Kiislamu linaloongoza Afghanistan.

Taliban, au "wanafunzi" ni lugha ya Kipashto , inayozungumzwa na Wapashtuni wa Afghanistan . Hawa waliibuka miaka ya 1990 kaskazini mwa Pakistan kufuatia kuondolewa kwa wanajeshi wa Umoja wa Kisoviet kutoka Afghanistan.

Viongozi wa kundi la Taliban wanatawala kwa mkono wa chuma na wanawake ndiyo waathirika wakubwa. Hivi karibuni wametangaza kibano kwa wanawake kinacholistua Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN) linaloingilia kati sakata la kinamama likilitaka taifa hilo kubadili sera zinazowalenga wanawake na wasichana na kuongeza wasiwasi wa mmomonyoko wa haki za binadamu.

Kundi la Taliban siku chache zilizopita lilipiga marufuku wanawake kusoma vyuo vikuu na kufanya kazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) hatua ambayo imesababisha asasi mbalimbali za misaada ya kibinadamu kusitisha utoaji wa huduma katika taifa hilo.

Kwa mujibu wa taarifa ya UN inayotolewa hivi karibuni, inastushwa na ongezeko la vikwazo vya elimu kwa kinamama na kutoa wito wa ushiriki kamili wa wanawake na wasichana katika taifa hilo la Asia ya Kati.

Baraza hilo linautaka utawala huo ambao umekuwa na vikwazo dhidi ya wanawake kufungua shule kwa wasichana na kubadili sera na mwenendo ambao unaongeza mmomonyoko wa haki za binadamu na uhuru wa kimsingi.

Taarifa hiyo pia inagusia marufuku ya wanawake kufanya kazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali na kuelezea matokeo mabaya zaidi kwenye operesheni za misaada ya kiutu katika taifa hilo.



Shekhe Mawlawi Hibatullah Akhundzada, kiongozi wa Taliban, anayetuhumiwa kuzuia kinamama wasionekane shuleni wala kazini. **PICHA:REUTERS.**

### UKIUKWAJI AHADI

Inaelezwa kuwa vikwazo hivyo vinakinzana na ahadi zinazotolewa na utawala wa Taliban kwa watu wa Afghanistan pamoja na matarajio ya jumuia ya kimataifa.

Katibu Mkuu wa UN Antonio Guterres, anaunga mkono ujumbe wa Baraza la Usalama, akitaja vikwazo vya hivi karibuni vilivyowekwa dhidi ya wanawake na wasichana kama ni ukiukwaji wa haki za binadamu usiovumilika, akisisitiza kwamba ni lazima kubatilishwa mara moja.

"Vikwazo vya hivi karibuni ni ukiukwaji wa haki za binadamu usio na uhalali, hatua za kuwatenga na kuwanyamazisha wanawake na wasichana zinaendelea kusababisha mateso makubwa na vikwazo vikubwa kwa uwezo wa watu wa Afghanistan," anasema na kuongeza:

"Jumuia ya kimataifa imekuwa ikiheshimu na kutoa kipaumbele kwenye utambuzi wake na kurejeshwa kwa misaada ya kibinadamu, huku haki za wanawake zikifanywa kuwa sharti muhimu katika mazungumzo na serikali ya Taliban," anasema Guterres.

Anaongeza kuwa marufuku ya wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu itakuwa na athari kubwa na ya haraka kwa shughuli za kibinadamu nchini humo ikiwa ni pamoja na kwa Umoja wa Mataifa.

### MATOKEO MABAYA

Kamishna Mkuu wa haki za Binadamu wa UN Volker Turk, anaonya kuhusu matokeo mabaya yatakayosababishwa na sera hizo akisema:"Hakuna nchi inayoweza kuendelea kijamii na kiuchumi huku nusu ya watu wake wakitengwa, vikwazo hivi visivyoeleweka vilivyowekwa kwa wanawake na wasichana sio tu vitaongeza mateso ya Waafghanistan wote, nahofia vitaleta hatari nje ya mipaka ya Afghanistan," anasema Turk.

Pia Turk anaonya kuwa kupiga marufuku wanawake kufanya kazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali kutazinyima familia zao mapato hasa wakati huu mahitaji ya kibinadamu yakiwa yameongezeka.

Aidha, anamulika pia namna ambavyo mashirika ya kiraia yatakavyodhoofika katika kufikia malengo yake, kwa kile alicho kitaja kuwa itaharibu uwezo wa mashirika hayo kutoa huduma muhimu.

Ofisa wa ngazi za juu wa misaada wa UN Martin Griffiths, aliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wiki iliyopita kwamba asilimia 97 ya Waafghanistan wanaishi kwenye umasikini.

Anabainisha kuwa karibu theluthi mbili ya watu wanahitaji misaada ili kuishi, huku wengine milioni 20 wakikabiliwa na hali mbaya ya njaa. Hata hivyo, inabainishwa kuwa katikati ya wimbi la uhitaji mkubwa wa mahitaji muhimu kundi la wasichana takriban milioni 1.1, lilipata pigo la kupigwa marufuku kwenda shuleni.

Vile vile inaelezwa kuwa tangu kundi la Taliban kutwaa mamlaka nchini Afghanistan, hivi karibuni walitoa pigo dhidi ya haki za wanawake baada ya kupiga marufuku wanawake kufanya kazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali.

Mashirika matano ya kimataifa yanayoendesha shughuli zake nchini humo, baada ya marufuku hiyo yalitangaza kisitisha shughuli zake katika taifa hilo lililoko chini ya viongozi wenye msimamo mkali, kwa kile walichosema kuwa itakuwa vigumu kuyafikia baadhi ya makundi ikiwemo wanawake na watoto wanaohitaji misaada.

Mashirika hayo ambayo ni Care International, Baraza la Wakimbizi la Norway (NRC) na Save the Children, yalisitisha kazi nchini Afghanistan baada ya wanawake kupigwa marufuku kuwafanyia kazi na serikali ya Taliban, wakieleza kuwa hawawezi kuendelea na kazi yao bila wafanyakazi wa kike.

Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji pia imesitisha huduma, huku Islamic Relief ikisema kwamba imekuwa inasimamisha kazi zake nyingi.

Inaelezwa kuwa tangu kutwaa tena udhibiti wa nchi hiyo, Taliban wameweka vikwazo kwa haki za wanawake licha ya kuahidi utawala wao utakuwa mpole zaidi kuliko utawala ulioonekana katika miaka ya 1990.

Pia pamoja na kupigwa marufuku kwa wafanyikazi wa NGO na wanafunzi wa kike wa vyuo vikuu kwa upande wa wanafunzi, ambayo sasa inatekelezwa na walinzi wenye silaha, shule za sekondari za wasichana bado zimefungwa katika majimbo mengi.

Wanawake pia wamezuiwa kuingia kwenye bustani na ukumbi wa michezo, ikiwa ni miongoni mwa maeneo mengine ya umma yanayoguswa na katazo hilo.

*DW Swahili*



## HABARI DODOMA

## Bashe awapongeza waandishi wa habari kuhabarisha umma kilimo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amewapongeza waandishi wa habari kutokana na kazi kubwa wanayoifanya kuhabarisha umma katika sekta ya kilimo hususan suala la utoaji mbolea ya ruzuku.

Alisema hayo jana wakati wa ufunguzi wa semina ya wahariri na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari inayoendelea jijini Dodoma yenye lengo la kuelimishana usalama wa chakula.

Alisema sekta ya habari ni muhimu sana kwenye jamii kwa sababu wanafichua upungufu uliojificha katika maeneo mbalimbali nchini.

"Nilipokuwa mikoa ya kusini hawa jamaa walikuwa wanahoji maswali ambayo yanakuonyesha sehemu kuna tatizo ikiwamo kukuelekeza kabisa," alisema Bashe.

Alisema jamii inapaswa kutambua umuhimu wa waandishi wa habari ikiwamo kuwatumia katika kazi za kuelimisha jamii kwenye maeneo mbalimbali nchini. Alisema wakifanya hivyo kila kitu cha maendeleo kitakwenda sawa katika maeneo ambayo mradi wa maendeleo unatekelezwa.

Akizungumzia semina hiyo, Bashe alisema ina umuhimu mkubwa kwa sababu inahusu masuala ya chakula.

Alisema, wizara imeamua kuandaa semina hiyo ili kuhakikisha wanahabari wanaandika kuhusu usalama wa chakula kwa jamii ili watambue umuhimu wa kuhifadhi chakula ili kuepukana na masuala ya sumukuvu.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Andrew Masawe, aliwataka waandishi kuendelea kuhabarisha umma kwenye sekta ya kilimo ili jamii iwe na uwelewa.

Alisema hakuna kitu muhimu kama kuhabarisha umma na waandishi wanapaswa kutumia kalamu zao kwa weledi ili kuhakikisha habari njema zinawafikia walengwa.

Mhariri Jane Mihanji kutoka Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) alimhakikishia Waziri Bashe kuwa jukwaa hilo litaendelea kushirikiana vizuri na wizara hiyo kwa sababu imeonyesha kutambua sekta ya habari.

Kadhalika, alisema wahariri watashirikiana vizuri na sekta ya kilimo kutokana na wizara hiyo kutambua umuhimu wao.

# Askofu aonya chuki za wazazi dhidi ya watoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma, Beatus Kinyaiya, amewataka wazazi kutotumia hasira za kuachana na wenza wao wanapowaonya watoto ili kuepuka kupandikiza chuki baina ya baba na watoto.

Askofu Kinyaiya, alitoa wito huo wakati wa Ibada ya Misa Takatifu ya Sakramenti ya Kipaimara kwa Wakristo 60, katika Parokia Teule ya Mtakatifu Cecilia-Muungano Jimbo Kuu Katoliki, Dodoma.

Alisema wapo baadhi ya kinamama wanapokorofishana na wenza wao, wanatoa adhabu zisizostahili kwa watoto kutokana na hasira jambo linalosababisha madhara makubwa kwa watoto na hata kupoteza maisha.

"Kwa namna ya pekee naomba kinamama msitumie hasira zenu kuumiza watoto mmekorofishana na bwana unakwenda kumalizia hasira kwa mtoto nalisema hilo kwasababu matukio ya namna hiyo yamekuwa yakitokea tena na tena.

"Kuna kinamama wanapiga watoto mpaka wanawaharibu wengine wanachukua wembe wana wachananachana. Ukimuuliza anakwambia nilikuwa na hasira kwa sababu ya baba yake sasa mama mtoto amekukosea nini, labda amekosea kidogo tu adhabu unayompa haiendani na kosa si sawa hiyo," alisema Askofu Kinyaiya.

Pia aliwataka kinamama kuacha kuchukua uamuzi wenye kuleta madhara kwa familia na hata jamii kutokana na hasira, inapotokea hali ya kutokuelewana baina yao na wenza wao.

"Naomba kinamama msipate hasira mkafanya mambo ambayo hayastahili, unapokuwa na hasira nakuomba usifanye maamuzi uwe baba au mama, padri au kiongozi usifanye maamuzi ukiwa na hasira."

"Unapotaka kufanya jambo ukiwa na hasira nenda chumbani ukajifungie usali na utulie, ukishatulia rudi utaamua tofauti na ulivyotaka kufanya hapo awali," alisema Askofu Kinyaiya.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, akipanda mti kando ya barabara jijini Dodoma jana, ikiwa ni Wiki ya Maadhimisho ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. **PICHA: OMR**

# Waziri aeleza athari za ukame nchini mwaka jana

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema ukame mkali ulikuwapo nchini katika kipindi cha mwaka jana umeleta athari nyingi ikiwamo mgawo wa maji, kupanda kwa bei za vyakula na vifo vya mifugo katika maeneo mengi.

Jafo, alibainisha hayo jana jijini hapo, alipokuwa akizindua upandaji miti katika sehemu ya maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema, kutokana na hali hiyo Watanzania wanatakiwa kuzitumia mvua za masika ambazo zinaendelea kunyesha hivi sasa kupanda miti ili kulinda mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Mwaka jana palikuwa na ukame mkali sana ambao ulisababishwa na mabadiliko ya tabianchi ambapo athari zake zimesababisha kupanda kwa bei ya vyakula kutokana na kukosekana kwa mvua za kutosha."

"Mvua haziji tu hivihivi lazima tutunze mazingira kwa kupanda miti katika maeneo yetu hasa katika vyanzo vya maji licha mgawo wa maji, lakini mgawo wa umeme ulikuwapo kutokana na vyanzo vyetu vingi vya kuzalisha umeme vinatokana na maji, pia mifugo katika maeneo mengi ilikufa kwa kukosa maji na malisho," alisema Jafo.

Vile vile, alisema kuelekea maadhimisho ya Miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar Januari 12, mwaka huu, matukio ya upandaji miti yataendelea ili kuhifadhi mazingira.

"Lazima tupande miti ili kuifanya Dodoma ya kijani na hii kampeni ya kukijanisha mkoa huu ilizinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa Makamu wa Rais mwaka 2017," alisema.

Aidha, aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha kuwa miti inapandwa katika vyanzo vya maji ili kuepuka mgawo.

"Mwaka huu katika wilaya zote tumepanga kupanda miti zaidi ya milioni 276, pia kupitia kampeni ya soma na mti tutapanda miti milioni 14.5 kwa kutumia wanafunzi ambao idadi yao nchi nzima wapo milioni 14.1," alisema Jafo.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Jabiri Shekimweri, alisema watahakikisha miti yote itakayopandwa katika Jiji la Dodoma, inatunzwa na kukua ili kuleta tija.

Aliwataka wakazi wa jiji hilo kuzingatia maagizo ya wilaya hiyo ya kila nyumba kupanda miti zaidi ya mitano ili kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



# Bashe: Hatutafunga mipaka bali tutaruhusu uuzaji wa mazao

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

SERIKALI imesema haitafunga mipaka bali itaendelea kuruhusu mazao yanayozalishwa na wakulima kuuzwa nje ya nchi kwa lengo la kuwahamasisha wananchi kuongeza uzalishaji.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe aliyasema hayo wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya wakati wa ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo zikiwamo skimu za umwagiliaji zinazoendelea kujengwa na serikali wilayani humo.

Alisema kitendo cha kuwazuia wananchi kuuza mazao yao nje ya nchi kwa kisingizio cha kuepusha upungufu wa chakula nchini kimekuwa kikiwakatisha tamaa wakulima kutokana na kutopata faida kwenye shughuli zao.

Alisema kitendo hicho kimekuwa kikisababisha bei ya mazao ya wakulima kushuka na kupanda bila utaratibu na hivyo wakulima kuzalisha kwa kubahatisha.

"Tunataka mazao ya wakulima yaendelee kuuzwa popote ambapo yatakuwa na soko zuri na tunataka bei za mazao zijirekebishe zenyewe, wakulima wakibaini mazao yao yana soko kubwa ndani na nje ya nchi wataongeza uzalishaji," alisema Bashe.

Alisema serikali itaendelea kuwaboreshea wakulima mazingira ya kuzalishaji ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya kilimo hasa umwagiliaji. Aidha, aliwataka wakulima wa Wilaya ya Mbarali wanaozalisha mpunga kwa kutumia skimu mbalimbali za umwagiliaji kuhakikisha wanalipa ada kila mwaka kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya skimu hizo.

Aliwataka wakulima hao kama hawako tayari kulipa ada hizo waseme ili serikali iache kuwekeza fedha kwa ajili ya miundombinu hiyo na badala yake ihamishie fedha kwenye miradi mingine ikiwamo ya elimu. Hata hivyo aliagiza Halmashauri ya Mbarali kushirikiana na wadau mbalimbali kuwapanga vizuri wananchi waliohamishwa kwenye vijiji vilivyokuwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ambao wameondolewa kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uhifadhi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema zimetengwa zaidi ya ekta 2,600 kwa ajili ya wananchi walioondolewa kwenye hifadhi na muda siyo mrefu wataanza kugawa kwa ajili ya wananchi hao kufanya shughuli zao.

Alisema eneo hilo limetengwa kwa ajili ya shughuli za kilimo na kwamba serikali itaweka miundombinu rafiki kwa ajili ya wananchi hao kuendelea na shughuli zao.

Homera alisema eneo hilo lilotengwa linatosheleza mahitaji ya wananchi wa vijiji vyote vilivyokuwa ndani ya hifadhi na hivyo akaeleza kuwa wanaandaa mkakati maalumu wa kuhakikisha wananchi wanaishi kwa amani kwenye maeneo yao.

"Tunaomba jambo hili lichukuliwe kama la dharura, lipimwe haraka na wananchi walioondolewa kwenye mashamba ya Madibila Two wapewe ili waendelee na shughuli zao maana huu ni msimu wa kilimo," alisema Homera.

Alisema ukubwa wa eneo hilo unatatosheleza wakulima wa eneo hilo pamoja na wa maeneo mengine wakiwamo walioondolewa kwenye eneo la Mnazi.

Baadhi ya wakazi wa Madibira walilalamika kuwa eneo hilo linalotajwa na serikali halitoshelezi mahitaji yao kwa maelezo kuwa likifanyika hivyo wataibua mgogoro mwingine.

Mmoja wa wananchi hao, Veronica Sofu alisema eneo linalotajwa wao wanalitumia kwa ajili ya kilimo cha mahindi na kwamba hata wao wenyewe haliwatoshi.



Baadhi ya wabunge wa Mkoa wa Mbeya (mstari wa mbele), wakifuatilia mawasilisho mbalimbali ya wataalamu kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa huo (RCC), jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mradi wa maji kuzinufaisha kaya 8,000 wilayani Rungwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya kaya 8,000 za Kijiji cha Mpandapanda Kata ya Kiwira wilayani Rungwe mkoani Mbeya zimeanza kunufaika na mradi wa maji wenye thamani ya Sh. milioni 500.

Mradi huo unazalisha lita milioni 19 kwa siku na umetekeleza kwa kutumia fedha za mpango maendeleo na mapambano dhidi ya UVIKO-19 na umejengwa kwa kutumia akaunti ya dharura.

Akizungumza baada ya kukagua na kuzindua tangi la maji lenye uwezo wa kuhifadhi lita 135,000, kiongozi wa mbio za mwenge kitaifa mwaka 2022, Sahili Nyazabara alisema miradi inayotekelezwa na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) ni fursa kwa wananchi.

Tangi hilo lililozinduliwa na kiongozi huyo linatarajiwa kusambaza maji katika vituo 16 vilivyosambazwa katika maeneo ya vijiji vinavyozunguka eneo hilo.

"Ni vizuri mkawa mnawapa wananchi elimu ili kuwa na utaratibu wa kulipa ankara za kila mwezi ili ziweze kuboresha miundombinu iliyo haribika," alisema Nyazabara.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, amesema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia jamii kupata huduma bora na kuchochea shughuli za kiuchumi hususani kilimo cha mboga.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, amewataka wananchi wa kata ya Kiwila kutoendelea na shughuli za kibinadamu kwenye chanzo cha maji.

**Tangi hilo lililozinduliwa na kiongozi huyo linatarajiwa kusambaza maji katika vituo 16 vilivyosambazwa katika maeneo ya vijiji vinavyozunguka eneo hilo.**

# RC aagiza wazazi kuchangia chakula shuleni kuongeza ufaulu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeagiza wazazi wote kuchangia chakula cha mchana kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi kwa lazima ili kuongeza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo jana kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) ambapo aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kutoa elimu kwa wananchi ili utekelezaji ufanyike kwa usahihi.

Alisema suala la chakula ni agizo la serikali na hivyo utekelezaji wake ni wa lazima kwa maeneo yote kwa maelezo kuwa baadhi ya maeneo watoto wanatoka mbali na shule na hivyo bila uwapo wa chakula cha mchana.

Alisema chakula cha mchana ni miongoni mwa mikakati ya serikali ya kuimarisha kiwango cha elimu nchini ikiwa ni pamoja na kuongeza ufaulu wa wanafunzi.

"Hili jambo ni la lazima na hivyo inatakiwa viongozi tukashirikiane kutoa elimu kwa wananchi wetu ili jambo hili litekelezwe kwa usahihi, wananchi bila kupewa elimu wanaweza wakatafsiri vibaya na ikaleta shida," alisema Homera.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, alisema suala la chakula cha mchana kwa wanafunzi ni utekelezaji wa Walaka wa Serikali Namba Tatu wa Mwaka 2016.

Alisema jambo hilo siyo la hiari na badala yake ni utekelezaji wa walaka huo, huku akisisitiza kuwa agizo hilo lilitokana na serikali kubaini kuwa wanafunzi wasipopata chakula cha mchana wanashindwa kusoma vizuri.

Alisema chakula hicho ambacho wazazi wanatakiwa kuchangia ni kile ambacho wangeweza kula hata wakiwa nyumbani na hivyo akaomba hamasa iongezeke.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, alishauri halmashauri zote kutunga sheria ndogo kwa ajili ya kusimamia utaratibu huo wa chakula kwa wanafunzi shuleni.

Alisema halmashauri zote mbili za Wilaya ya Rungwe ambazo ni Rungwe na Busokelo, zimeanza kutekeleza utaratibu huo ambao alisema una tija kwenye sekta ya elimu.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera aliagiza halmashauri zote za mkoa huo kujenga shule maalumu za msingi zenye mchepuo wa Kiingereza pamoja na shule za sekondari ambazo zitakuwa zinapokea wanafunzi wanaotoka kwenye shule hizo.

Vilevile aliagiza halmashauri kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa mabweni kwenye shule za sekondari kwa ajili ya wasichana ili kuwaepusha na matatizo mbalimbali ikiwamo kulaghaiwa na 'mafataki'.

Kaimu Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Amos Helen, alisema kwa mwaka huu mkoa umefikia asilimia zaidi ya 70 ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali na asilimia zaidi ya 80 kwa wanafunzi wa darasa la kwanza.

Alisema mkoa huo una mikakati mbalimbali ya kuimarisha sekta ya elimu kwa kuboresha uongozi katika ngazi zote pamoja na kuboresha miundombinu ya shule.



# ZRB kuendesha operesheni ya kamata waongoza watalii 'feki'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BODI ya Mapato Zanzibar (ZRB) imesema inatarajia kufanya operesheni ya kuwasaka waongoza watalii ambao hawajasajiliwa kisheria na hawalipi kodi.

Imesema kwa yeyote ambaye atabainika atapewa adhabu kali kwa mujibu wa sheria.

Kamishna wa ZRB, Yusuphu Juma Mwenda aliyasema hayo jana wakati akifunga kikao cha tathmini ya utendaji kazi kwa watendaji wa bodi hiyo.

Alisema wapo baadhi ya watu wanafanya kazi hiyo kinyume na sheria na kusababisha kutokuwapo kwa usawa katika ulipaji wa kodi kwa sababu wapo ambao wamesajiliwa kisheria na wanalipa kodi.

Alisema bodi hiyo inakusudia kukusanya kodi ya Sh. bilioni 300 katika miezi sita ijayo hasa katika maeneo ambayo hayaleti usawa katika ulipaji wa kodi ikiwamo katika sekta ya utalii kwa upande wa waongoza watalii.

"Kuna watu wanafanya shughuli hizo bila ya kujisajili wala kulipia kodi wakati zipo kampuni zinazofanya kazi hiyo yaliosajiliwa na kulipa kodi,"alisema Kamishna huyo.

Kamishna huyo alisema mapato wanayokusanya zaidi ya asilimia 50 yanatokana na sekta ya utalii, hivyo ni lazima kuhakikisha kila anayestahili kulipa kodi kulipia.

Alisema wapo baadhi ya watu wanafaidika kwa uwapo wa utalii Zanzibar lakini wale wanaolipa kodi wasionewe na wachache wasiolipa kodi.

Alisema miezi sita iliyopita bodi hiyo ilikusudia kukusanya Sh. bilioni 290 lakini walikusanya Sh. bilioni 286.

Aidha, alisema wataendelea kutoa elimu ya ulipaji wa kodi kwa jamii na wafanyabiashara ili kila anayestahiki kuchangia kodi achangie kulingana na sheria ilivyo.

Hata hivyo alisema ujio wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar badala ya bodi ya mapato unalenga kutoa huduma bora kwa walipa kodi, kuwasikiliza walipa kodi, kushirikiana nao kuondoa matatizo na kurahisisha biashara zao.

Alisema hivi karibuni wanatarajia bodi hiyo itabadilika na kuwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), hivyo wananchi wasiwe na hofu ya mabadiliko hayo na kuendelea kulipa kodi na kudai risiti kila wanapofanya manunuzi.

Ofisa Leseni kutoka Kamisheni ya Utalii, Muhammed Walid Fikirini, alisema wamejipanga kuzuwia waongoza utalii wanaofanya kazi kinyume na sheria, hivyo aliwataka wadau wa utalii kufuata taratibu za serikali ili kupeleka gurudumu la maendeleo mbele.

"Waongoza utalii wamegawika katika sehemu tofauti wapo ambao ni wenyeji wa Zanzibar na hawana vibali vya kutembeza watalii lakini kumejitokeza wimbi la baadhi ya wawekezaji ikiwamo mameneja wa hoteli wanafanya kazi hiyo ya kuwatembeza watalii katika vivutio vya utalii jambo ambalo ni kinyume na sheria,"alisema.

Meneja wa Ukusanyaji Kodi ZRB, alisema milango ya bodi hiyo ipo wazi kwa wafanyabiashara ambao wanamalalamiko kuhusu ulipaji wa kodi.

"Kama kuna mfanyabiashara yeyote ambaye anahisi amewekwa katika eneo ambalo hastahiki kuwapo milango ya ZRB ipo wazi kupeleka malalamiko yao ili kushughulikiwa," alisema.

Mkurugenzi wa Marejesho na Makusanyo ya Mapato ZRB, Shabani Yahya Ramashan, alisema matatizo ya kiutendaji katika miezi sita iliyopita kutofikia asilimia 100 ya ukusanyaji wa mapato kulisababisha baadhi ya wafanyabiashara kutotoa risiti na baadhi ya wanaotoa kufanya udanganyifu wa mauzo.

Mkurugenzi wa ZRB Kisiwani Pemba, Jamal Hassan Jamal, alisema wamejipanga kuzuia mianya ya ulipaji wa kodi ili kupindukia asilimia 100 ya ukuasanyaji wa mapato ambapo bodi hiyo katika miezi sita iliyopita ilifikia asilimia 99.



Vijana wa UVCCM wakipita mbele ya Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani), katika shamrashamra za miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika Kijiji cha Paje, Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# 'Maonyesho ya Biashara Mapinduzi yafungua fursa za huduma'

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amesema maonyesho ya tisa ya biashara ya mapinduzi yanawapa fursa wananchi kupata huduma katika eneo moja kuliko awali walikokuwa wanazifuata mbali.

Aliyasema hayo alipotembelea maonesho hayo katika Viwanja vya Maisara Mjini Zanzibar.

Akiwa katika maonyesho hayo aliipongeza Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kuyaboresha maonesho hayo.

Alisema maonesho hayo ni ya aina yake hasa kuona washiriki wa Zanzibar na nchi mbalimbali, kwamba kuongezeka kwa ushiriki wao kuonyesha kuwapo kwa maandalizi mazuri yanayosimamiwa na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

Aidha, aliwataka wananchi kujitokeza na kutembelea taasisi za serikali zinazotoa huduma pamoja na kupata maelekezo kuhusiana na huduma wanazozitoa.

Hemed alifurahishwa kuwapo kwa kituo jumuishi katika maonesho hayo ambacho kinajumuisha taasisi mbalimbali zilizoshiriki na kueleza kuwa uwapo wa kituo hicho kunaonesha ushirikiano uliopo baina ya taasisi mbalimbali.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaban, alisema wizara itaendelea kuchukua maelekezo watakayopatiwa na viongozi wanaokuja kutembelea kwa lengo la kuboresha maonyesho hayo.

## SMZ yaanika mikakati ya kuwakomboa wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imeweka mikakati ya kuwawezesha wajasiriamali kujikomboa na kupiga hatua ya maendeleo, kiuchumi katika uzalishaji wa asali kuingia katika soko la kimataifa.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Maendeleo ya Ardhi na Makazi, Rahma Kassim Ali, wakati akiweka jiwe la msingi Kituo cha Kusarifu na Uzalishaji wa Asali kilichoko Kizimbani Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema serikali imetenga fedha nyingi zikiwalenga wajasiriamali wanawake kufanya shughuli zao kwa lengo la kupambana na umaskini.

Alisema kwa mara ya kwanza serikali imetenga fedha kwa ajili ya wajasiriamali wazalishaji wa asali baada ya kuona juhudi zao zinafanyika bila ya utaalamu.

Alisema hivi sasa mahitaji ya soko la asali ni kubwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambapo wazalishaji hao nafasi yao ni kubwa ya kujikomboa.

"Uwekaji jiwe la msingi katika kituo cha usarifu wa uzalishaji wa asali kwa kiasi kikubwa lengo lake ni kuwakomboa wajasiriamali wanawake kuona kwamba wanapiga hatua kubwa ya maendeleo ya kiuchumi na kuingia katika soko la asali ambalo ni kubwa ikiwamo katika sekta ya utalii," alisema.

Aidha, aliwataka wajasiriamali wafugaji wa nyuki kuzalisha asali yenye ubora ambayo itatokana na utaalamu wanaoupata kupitia vituo mbalimbali vya uzalishaji wa asali.

Akizungumza katika uzinduzi wa kituo hicho, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema katika fedha za UVIKO-19, Serikali imetenga Sh.bilioni 36 kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Aidha, alisema kwa mara ya kwanza serikali imetenga Sh.milioni 280 kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali wanaojishughulisha na uzalishaji wa asali ambao wamepatiwa mikopo hiyo.

Katibu Mkuu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji, Mariyam Abdalla Sadalla, alisema tayari vikundi vya uzalishaji wa asali vimepatiwa mafunzo na vifaa ambavyo vitawawezesha kuzalisha asali yenye viwango itakayoingia katika ushindani wa soko.

Mmoja wa wazalishaji wa asali katika Kijiji cha Bwejuu katika Wilaya ya Kusini Unguja, Salma Haji Mwadini, alisema matarajio yao ni kuona kituo kinayafikia malengo ya uzalishaji wa asali bora yenye viwango.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**WILHELMI VALENTINE TESHA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0508/0106 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Mlama Secondary mwaka 2016. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0629/0698 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Edmund Rice Sinoni Secondary mwaka 2019. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **AR/RB/134/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BARAKA MOHAMED LUWUMBA ANATANGAZA** kupotelewa na kadi ya **GARI (MITSUBISHI)** yenye namba za usajili **T 196 ADT**

Chasis Namba: **FK417K540906**

Engine Namba: **6D16617462**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/14090/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya DODOMA**

**Kituo cha MJINI DODOMA Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai Na. 128/2022**

**Jina la Mdai............SAMWEL S. MWITA**

**Jina la Mdaiwa ................ SAMBA PUNUTA**

**AMRI YA KUUZA MALI KUTIMIZA HUKUMU**

**(Kanuni ya 72, 73 & 78 ya kanuni za Utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa ROYAL RUNNERS (BENSON A. CHAMLESILE)**
**BOX 10485 DODOMA**
**KK kwa Hakimu Mkazi Mfawidhi**
**Mahakama ya Wilaya**

Kwa hati hii nakuamuru kuuza katika mnada wa hadhara baada ya kutangaza kwa muda wa siku 21 kwa kubandika katika mbao za matangazo na Nyumba ya mdeni Mhukumiwa ikieleza wakati na mahala patakapo fanywa mnada huu na mali itakayouzwa, na baada ya kutangazwa mali ambayo ni GARI No. 332 BRE iliyokamatwa kwa hati ya kukamatia mali iliyotolewa na Mahakama hii tarehe 2 Mwezi 11 mwaka 2022 kwa kutimiza hukumu ya mdai aliyetajwa hapo juu, au mali itakayokamilisha kiasi cha shilingi 6,700,000/= Unaamriwa tena kurudisha hati hii kabla ya tarehe 06/01/2023 ikiwa na maandishi yako ya kuthibitisha namna amri ilivyotekelezwa au kwanini haikutekelezwa.
Endapo mdeni mhukumiwa atalipa na kuthibitisha kiasi kinachodaiwa na gharama zote za mnada kabla ya tarehe ya mnada, mnada wa mauzo utasitishwa.

**ORODHA YA MALI INAYOTAKIWA KUUZWA**
**KUUZA GARI NO. T322 BRE NA KUMLIPA MDAI SHILINGI 6,700,000/=**
Hati hii yatolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama leo tarehe 15/12/2022

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI NA. 124 YA 2020**

**GRACE SIMON NOHA ..........................................MDAI 1**
**VEISI SIMON NOHA .......................................... MDAI 2**

**VERSUS**

**ELIA RICHARD KISABUJE ..........................................MDAIWA 1**
**LOSHIPAY LAIZER .......................................... MDAIWA 2**
**GREYSON SIBONA .......................................... MDAIWA 3**
**TIDAYA KIYENGULA .......................................... MDAIWA 4**
**BLANDINA SAMWEL MKAMBA .......................................... MDAIWA 5**

**KWA: LOSHIPAY LAIZER**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 06.02. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 10 ya mwezi wa JANUARI, 2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAVID LAURENT WANG'ANYI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 410 DFV – TOYOTA COROLLA.** Chassis namba **AE1105200727.** Engine namba **EA200727.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/OST/RB/6539/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

## TAARIFA KWA UMMA

Kampuni ya **PMM ESTATES (2002) LTD** itasafirisha mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda **PMM ICD** Vingunguti kwa kutumia gari zenye namba za usajili

**T274DQV/T472CVG,**
**T281DQV/T473CVG,**
**T614DVW, T799DVW**

**Vipimo ni kama ifuatavyo:**
Urefu mita 18
Upana mita 4.90
Kimo mita 4.80

Safari imepangwa kuanza tarehe 10.01.2023

Njia zitakazotumika ni Mandera Road na Nyerere Road.

Gari zitasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni.

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

**REGISTRATION OF DOCUMENT ACT**
**(CAP.117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEP POLL**

**By THIS DEED.I EMANUEL LAURENCE PAUL** of Dodoma, formerly known as **HALID LAURENCE PAUL .DO HEREBY** absolutely renounce and abandon the use of my former names **HALID LAURENCE PAUL** in lieu thereof assume and adopt as from the date hereof the name of **EMANUEL LAURENCE PAUL.**
**AND IN PURSUANCE** of such change of name aforesaid, **I HEREBY DECLARE THAT,** I shall at all times hereinafter in all records, deeds, transactions, instruments, proceedings, dealings, in writing and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of **EMANUEL LAURENCE PAUL** as my name in lieu of the said names of **HALID LAURENCE PAUL** renounced as aforesaid.
**AND I HEREBY AUTHORISE and REQUEST** all persons to designate and address me in the name of **EMANUEL LAURENCE PAUL.**
**I, EMANUEL LAURENCE PAUL** makes this declaration conscientiously believing the same to be true and in accordance with the provisions of The Oaths (Judicial Proceedings and Statutory Declarations) CAP 34 R.E.2002
**IN WITNESS WHEREOF** I hereunto set my subscribed the name of **EMANUEL LAURENCE PAUL** on the day and in the manner hereinafter appearing.

**SIGNED and DELIVERED** at Dodoma by the said **EMANUEL LAURENCE PAUL** who is known to me personally this 21st day of December, 2022. } **DEPONENT**



**BEFORE ME:**
Name:
Signature:
Qualification: Commissioner for Oath's

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YAHAYA JUMA MGOLI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T967DQV** aina ya **Toyota IST,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/13673/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha DODOMA MJINI**
**Shauri la Madai/Ndoa Na.129/2022**

**Jina la Mdai AMINA RASHID MGWALE**
**Jina la Mdaiwa ERICK NELWIN ZABLON**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa ERICK NELWIN ZABLON**
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba **KUOMBA TALAKA, MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO**
Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 16 Mwezi 01 Mwaka 2023 Saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wake na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea
**ANGALIZO**:Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 02 Mwezi 01 Mwaka 2023.**

PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

..................................................
**HAKIMU**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LTD,** Sisi **RAISSA COMPANY LTD** tunatangaza mnada wa hadhara wa kuuza mali (dhamana) za mdaiwa sugu aliyekopa na kushindwa kulipa deni lake. Mnada utaendeshwa yard ya Makumbusho kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdaiwa/ Mdhamini | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| EVELYN SHIJA KABELELA | Home Chattels (Vitu vya ndani) | 24.01.2023 |
| Biswaro Zebedayo Msase | Home chattels (Vitu vya ndani) | 24.01.2023 |

**Mashati Mengine:-**
Mnada utafanyika makumbusho yard mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi. Gharama za kubeba mali iliyouzwa ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**RAISSA CO LTD Phone no. 0652113262**
**Tujijenge (TZ)+255 222774742-3/0677024661**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Nyaraka za siri zakutwa ofisini kwa Rais Biden

**WASHINGTON, Marekani**

IKULU ya Marekani imesema idara ya haki ya nchini humo inachunguza nyaraka za siri zinazodaiwa kupatikana katika ofisi ya zamani ya Rais Joe Biden.

Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa jana na BBC, takriban mafaili 10 kati ya nyaraka hizo zilikutwa zimefungiwa mahali katika Kituo cha Penn Biden huko Washington mwezi Novemba na timu ya wanasheria wa Biden, na kwamba nyaraka hizo zimekabidhiwa kwa hifadhi ya taifa.

Inaelezwa kwamba mtangulizi wa Biden, Donald Trump, na yeye anakabiliwa na uchunguzi wa kupeleka faili za siri Florida baada ya kumaliza urais wake.

Kwa mujibu wa CBS News, FBI inahusika katika uchunguzi wa nyaraka za siri zilizopatikana katika kituo cha Penn Biden, na kubainishwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Marekani Merrick Garland ametakiwa kupitia nyaraka hizo.

Chanzo kinachofahamu suala hilo kiliiambia CBS News kuwa nyaraka hizo hazikuwa na siri za nyuklia na zilikuwa zimewekwa kwenye sanduku lenye karatasi zingine ambazo hazijaainishwa.

Richard Sauber, wakili maalum wa Rais Biden, alisema kwamba faili ziligunduliwa kabla ya uchaguzi wa katikati ya muhula na mawakili wa Biden ambao walikuwa wakihamisha vitu.

Inaelezwa kuwa Biden aliweka ofisi hiyo katika jumba ambalo liko maili moja kutoka Ikulu ya White House, akiwa hapo kuanzia mwaka 2017 hadi 2020.

Aidha, inatajwa kuwa Trump mwanzoni mwa wiki hii kwenye mtandao wa kijamii aliandika akiuliza "Ni lini FBI itavamia nyumba nyingi za Joe Biden, labda hata Ikulu ya Marekani?"

*BBC*



Wanajeshi nchini Brazil wakivunja kambi za wafuasi wa raisi wa zamani wa nchini humo, Jair Bolsonaro. **PICHA: DW.**

# Kambi wafuasi wa Bolsonaro yavunjwa Brazil

**BRASILIA, BRAZIL**

POLISI nchini Brazil imevunja kambi za waandamanaji na kuwakamata zaidi ya watu 1,500 siku moja baada ya wafuasi wa rais wa zamani Jair Bolsonaro kuyavamia majengo ya utawala.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na DW, mamia ya wanajeshi na polisi walitawanywa kwenye mji mkuu Brazilia kuzivunja kambi kadhaa za waandamanaji nje ya Makao Makuu ya jeshi la nchi hiyo.

Inaelezwa kuwa kwenye eneo hilo kulikuwa na wafuasi 3,000 wa rais wa zamani Jair Bolsonaro waliofunga mahema yaliyotumika kama kambi kwa maelfu ya waandamanaji walioyavamia majengo muhimu ya utawala mjini Brazilia juma lililopita.

Operesheni hiyo imefanyika baada ya Mahakama ya Juu ya Brazil kutoa amri ya kuondolewa kambi zote za waandamanaji kutokana na uvamizi ulioyalenga majengo ya Bunge, Mahakama ya Juu na Ikulu.

Polisi pia ilisema imewakamata zaidi ya waandamanaji 1,500 wanaohusishwa na uvamizi huo ulioongozwa na wafuasi wa Bolsonaro ambao wanayapinga matokeo ya uchaguzi wa Oktoba 2022, yaliyomnyima ushindi mwanasiasa huyo wa mrengo wa kulia na kushinda Rais Luiz Inacio Lula da Silva.

Pia ilibainishwa kuwa Mahakama ya Juu ya nchi hiyo imewaondoa madarakani kwa muda wa siku 90 gavana wa jimbo la Brazilia, Ibaneis Rocha.

Kiongozi huyo anayehisiwa kuwa na ukaribu na Bolsonaro anatuhumiwa kutochukua hatua za kuimarisha usalama licha ya ishara zote za tahadhari zilizoonekana kabla ya uvamizi.

Tangu kutokea mkasa huo kumekuwa na ukosoaji mkubwa ndani na nje ya Brazil, na kwamba jana mamia ya watu walikusanyika katikati ya mji wa Sao Paulo kwa maandamano ya kuilinda demokrasia na kushinikiza kuchukuliwa hatua kwa wote waliovamia majengo ya serikali.

Waandamanaji hao wakiwemo vijana watetezi wa haki za wafanyakazi na wanaharakati wanaopinga ubaguzi wa rangi walionekana mtaani wakiwa na mabango yaliyosomeka "Tuko pamoja na Lula na kwa ajili ya demokrasia" mengine yakisomeka "heshimu kura ya umma".

Kwa mujibu wa DW, jana jioni Rais Lula alirejea ofisini kwake kwa mara ya kwanza tangu uvamizi wa mwishoni mwa juma, na kwamba alifanya mkutano wa usalama na magavana 20, huku akirudia ahadi yake ya kuwasaka wote waliohusika na vurugu ya Januari nane.

*DW*

## Raia 24 wauawa na waasi DRC

**KINSHASA, DRC**

WAASI wanaodhaniwa kuwa ni kutoka kundi la CODECO, wamewauwa watu zaidi ya 24 mwishoni mwa juma lililopita katika vijiji kadhaa kwenye jimbo la Ituri, mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kwa mujibu wa mashirika ya kiraia kwenye eneo hilo, waasi hao walishambulia eneo la Djugu, na kuchoma moto nyumba na kuharibu mali nyingine ikiwemo kutekeleza mauji.

Mashirika hayo yalisema, miili mingi ilipatikana katika vijiji vya Jisa, Largu na Blukwa kaskazini mwa jimbo hilo, licha ya baadhi ya maeneo kutofikiwa, huku idadi ya vifo ikitajwa huenda ikaongezeka.

Hata hivyo madai hayo ya mashirika ya kiraia yamekanushwa na msemaji wa jeshi kwenye eneo la Ituri, Luteni Jules Ngongo, ambaye mbali na kuthibitisha tukio hilo alisema ni watu wanne ndio walifariki akiwemo mwanajeshi mmoja.

Mwanaharakati mmoja wa kutetea haki za binadamu kwenye eneo hilo, Desire Mbutchu, aliliambia shirika la habari la AFP kuwa, waasi wa CODECO walitekeleza mashambulio hayo kama ulipizaji kisasi kwa madai ya kuuawa kwa mwalimu kutoka jamii ya Lendu, ambayo kwa muda sasa wamekuwa katika mzozo na jamii za watu wa Hema.

*RFI*

## Ukosefu usalama watabiriwa kuathiri uchaguzi Nigeria

**ABUJA, Nigeria**

TUME ya uchaguzi nchini Nigeria imesema uchaguzi mkuu wa mwishoni mwa mwezi Februari unaweza kufutwa au kuahirishwa ikiwa ukosefu wa usalama hautashughulikiwa.

Inaelezwa kuwa Rais Muhammadu Buhari ambaye ataachia ngazi baada ya kuhudumu mihula miwili, anaondoka madarakani bila kumaliza uasi wa miaka 13 wa wanamgambo wa Kiislamu eneo la Kaskazini Mashariki.

Aidha, inadaiwa kuwa bado kuna ongezeko la uhalifu mbaya Kaskazini Magharibi na katika majimbo ya katikati mwa nchi hiyo, pamoja na mivutano ya kujitenga kusini mashariki.

Mwenyekiti wa tume huru ya kitaifa ya uchaguzi, Abdullahi Zuru, alisema "Ikiwa ukosefu wa usalama hautafuatiliwa na kushughulikiwa kwa uthabiti, mwishowe unaweza kusababisha kufutwa au kuahirishwa kwa uchaguzi katika maeneo bunge mengi na kudhoofisha kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi".

Pia alisema hali hiyo inaweza kuchochea mzozo wa kikatiba, akisisitiza kuwa lazima hali hiyo isiruhusiwe kutokea na haipaswi kuruhusiwa kutokea.

*VOA*

# KAPOMBE ATOA AHADI NZITO KWA ROBERTINHO

**Na Hadija Mngwai**

BEKI Mkongwe wa Simba, Shomari Kapombe, ametoa ahadi nzito mbele ya kocha mpya wa timu hiyo, Mbrazil Robertinho Oliveira kuwa watahakikisha wanashinda kila mchezo uliopo mbele yao wa Ligi Kuu na kimataifa ili kutimiza malengo yao na kocha.

Simba imeweka kambi ya wiki moja Dubai, Falme za Kiarabu, ikijiandaa na Ligi Kuu, Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo pia ni wakati maalum kwa Robertinho kuwasoma wachezaji wake vema baada ya kujiunga na timu hiyo mapema mwezi huu.

Akizungumza Nipashe kutokea Dubai, Kapombe alisema wanahitaji kuungana pamoja kutimiza malengo yao na ya kocha kwa kuhakikisha wanajituma ipasavyo ili kuweza kushinda kila mchezo ulio mbele yao.

"Tunashukuru viongozi kwa kuweza kutufikisha hapa, 'facility' (sehemu ama vifaa) zote zinaturuhusu kufanya mazoezi kwa bidii, wachezaji tupo vizuri na mwalimu amezidi kutupa madini yake yatakayotusaidia katika ligi na kimataifa.

"Kambi hii ni nzuri kwetu kwani imetuweka pamoja baada ya kuwa katika makundi mawili wengine walikuwa kwenye michuano ya Mapinduzi na wengine mapumziko, hivyo ni kambi sahihi inayotufanya tuwe karibu na mwalimu ambayo inamsaidia kujua tabia ya kila mchezaji na kujua anahitaji nini hivyo itatusaidia.

"Mazoezi anayotoa mwalimu ni ya kiwango cha juu sana kila mchezaji anajitolea kwa kujituma, pia mwalimu kuna vitu ametueleza kama malengo yake na vitu vizuri ameviona kwetu atatusaidia, kocha amesema Simba ni timu kubwa yenye malengo, hivyo tupambane kwani amekuja kushinda.

"Hivyo sisi kama wachezaji tutajiandaa kushinda katika kila mechi ili tumsaidie mwalimu kutimiza malengo, hivyo inatupa changamoto ya kushinda kila mchezo ulio mbele yetu," alisema na kuongeza;

" Mwalimu ametuelezea malengo yake na mafanikio aliyoyapata alipotoka, hivyo ametupa changamoto na chachu kwetu wachezaji ya kupambana."

Jaribio la kwanza la Robertinho kwenye mechi za mashindano akiwa na Simba litakuwa mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Mbeya City katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumanne ijayo kabla ya kuifuata Dodoma Jiji Januari 22 na kisha kurejea Dar es Salaam kuikaribisha Singida Big Stars Februari 3, mwaka huu.

Baada ya mechi hiyo, ataiongoza Simba kwenye mechi ya kwanza ya hatua ya Makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika ugenini nchini Guinea kuvaana na wenyeji wao, Horoya AC.

**SASA NI SAMBA!!!...**



Rais wa Heshima wa Simba na Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji (kulia), akisalimiana na Kocha Mkuu mpya wa timu hiyo, Mbrazil Robertinho Oliveira, baada ya kukutana na kuzungumza na wachezaji pamoja na benchi la ufundi katika kambi yao huko Dubai jana. **PICHA: SIMBA**

## Polisi yampa mwaka Mkongo wa Zahera

**Na Hadija Mngwai**

TIMU ya Polisi Tanzania imempa mkataba wa mwaka mmoja mshambuliaji Mayala Enock raia wa DR Congo, ambaye ni chaguo la Kocha wao mpya, Mwinyi Zahera, katika dirisha hili dogo la usajili.

Polisi Tanzania ipo mkiani mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara hivyo inahitaji kujinasua katika nafasi hiyo, ambapo inatumia dirisha hili dogo la usajili kujiimarisha zaidi.

Zimebaki siku nne kuanzia leo kabla ya dirisha hilo kufungwa Januari 15, mwaka huu, jambo ambalo timu mbalimbali zinazoshiriki ligi hiyo, zimekuwa katika harakati nzito ya kusaka nyota wakuwasaidia kufikia malengo yao.

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu Msaidizi wa Polisi Tanzania, Michael Ntebezi, alisema tayari wameshafanikiwa kumpa mkataba nyota huyo wa kimataifa DR Congo huku wakiwa wamebakisha nafasi mbili za usajili mpya.

"Tunaendelea na usajili wa baadhi ya wachezaji wakongwe ndani ya timu yetu ili tukamilishe mchakato katika dirisha hili dogo, kuna wachezaji wawili ambao tulishawaongeza kwenye kikosi chetu ambao ni Mohamed Issa Banka na Ramadhani Ridondo.

"Pia nyota wetu Mkongo Mayara Enock, tumempa mkataba wa mwaka mmoja ambapo kwa sasa tunaendelea kufuatilia ITC yake kwa kuwa usajili unaotumika ni wa TMS, hivyo tukikamilisha ataanza kuitumikia timu yetu.

"Kwa sasa tumebakiza nafasi mbili za kusajili ili tukamilishe usajili ambao ni wa beki wa pembeni na winga mmoja, tunahitaji kusajili wachezaji wakongwe ili waweze kuisaidia timu," alisema Ntebezi.

# Simba Queens, Mkwawa Queens vitani leo

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Wanawake cha Simba, Simba Queens, leo kinatupa karata yake nyingine ya kuwania pointi tatu muhimu kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara dhidi ya wenyeji wao, Mkwawa Queens.

Mchezo huo utakaopigwa katika Uwanja wa Samora mjini Iringa, unatarajiwa kuwa mgumu na wenye ushindani kutokana na ubora wa timu zote mbili, kila moja ikihitaji alama tatu ili kujiweka pazuri katika ligi hiyo.

Malkia wa Wekundu wa Msimbazi hao, watashuka dimba kwa tahadhari kubwa kuhakikisha wanapata pointi muhimu katika mchezo huo wa ugenini ikiwa ni baada ya kushinda mechi iliyopita kwa mabao 2-1 dhidi ya vinara wa ligi hiyo, Fountain Gate.

Kuelekea mchezo huo Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amesema kikosi chake kipo kwenye hali nzuri na morali ya wachezaji ipo juu tayari kuhakikisha wanapambana kupata alama tatu. Alisema ushindi waliopata katika mechi iliyopita dhidi ya Fountain Gate Jumanne iliyopita, umeongea ari kwa wachezaji ambao anaamini utawafanya kusaka tena ushindi.

"Tumewasili salama Iringa na tayari kwa mchezo wetu wa kesho (leo) dhidi ya Mkwawa Queens, tunatarajia utakuwa mchezo mgumu, lakini tumejipanga kuhakikisha tunashinda. "Ligi ya msimu huu ni ngumu, ushindani umeongezeka kila timu imejiandaa vizuri, lakini sisi ni mabingwa watetezi, hivyo tunahitaji kufanya vizuri kwenye kila mchezo," alisema Lukula.

Alisema licha ya ugumu wa ligi wamejipanga vizuri kuhakikisha wanapambana kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huo ili kufikia malengo ya kutetea mataji yao.

"Mipango yetu ni kutafuta matokeo mazuri katika kila mchezo, tunaingia kwa tahadhari na kuwaheshimu wapinzani wetu kwani ni wazuri, licha ya kushika mkia katika msimamo wa ligi," alisema kocha huyo.

Alisema kushika nafasi ya chini ya msimamo haina maana ni timu mbovu, hivyo hawataidharau kwa sababu mpira wa miguu ni mchezo wa makosa na wanaweza kupoteza mbele ya timu hiyo wasipokuwa makini.

Simba Queens ambao ni mabingwa watetezi, wapo nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi saba baada ya michezo minne wakishinda mbili, sare moja na kupoteza mmoja dhidi ya JKT Queens ambao wanaongoza msimamo wakiwa na pointi 10.

Michezo mingine itakayopigwa leo ni kati ya Amani Queens na Jkt Queens katika Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi na Fountain Gate Princess dhidi Alliance Girls, katika dimba la Jamhuri Dodoma.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WEGHORST KUJILIPIA KUHAMA

MSHAMBULIAJI wa Burnley na Uholanzi, Wout Weghorst, mwenye umri wa miaka 30, ambaye yuko kwa mkopo Besiktas, amejitolea kulipa ada ya fidia kwa klabu hiyo ya Uturuki kutoka mfukoni mwake ili kulazimisha kuhamia Manchester United na huenda akakamilisha uhamisho huo kufikia leo. ***(Gokhan Dinc via Express)***

### ENZO BASI TENA

KOCHA wa Benfica, Roger Schmidt, amesema harakati za Chelsea za kumnasa kiungo wa Argentina, Enzo Fernandez, ambaye mkataba wake una kipengele cha gharama kuuzwa kwa takriban pauni milioni 106 "zimefungwa". ***(Mirror)***

### JOAO MKATABA MPYA

KLABU ya Atletico Madrid inataka kuongeza mkataba wa mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix, kwa mwaka mmoja zaidi hadi 2027 kabla ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, kujiunga na Chelsea kwa mkopo kwa kipindi cha msimu uliosalia. ***(Marca)***

### THURAM NA CHELSEA

CHELSEA wameongeza kasi kwenye mbio zao za kutaka kumnunua mshambuliaji wa Borussia Moncheng-ladbach, Marcus Thuram mwenye umri wa miaka 25, ambaye mkataba wake unamalizika majira ya joto. ***(Mail)***

### MADUEKE KUNG'OLEWA PSV

KLABU ya Chelsea pia inafikiria kumnunua mshambuliaji wa PSV Eindhoven na Timu ya Taifa ya England chini ya miaka 21, Noni Madueke, mwenye umri wa miaka 20. ***(Times)***

### EN-NESYRI ATAKIWA

KLABU ya West Ham United imeonyesha nia yao ya kumnunua mshambuliaji wa Sevilla, Youssef En-Nesyri na wanatumaini kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco mwenye umri wa miaka 25 kwa mkopo kwa muda wa miezi 6. ***(Watch)***

### BRIGHTON YAKATAA OFA HEWA

KLABU ya Brighton imekataa ofa ya maneno kutoka kwa Tottenham Hotspur kwa ajili ya mshambuliaji wa Ubelgiji, Leandro Trossard, mwenye umri wa miaka 28. ***(Football Insider)***

### RUTTER AWINDWA LEEDS

LEEDS United iko kwenye mazungumzo ya mwisho ya kumsajili mshambuliaji Mfaransa Georginio Rutter, mwenye umri wa miaka 20 katika uhamisho wenye thamani ya hadi pauni milioni 35.3 kutoka Klabu ya Ujerumani ya Hoffenheim. ***(Sky Sports)***

### GELHARDT KWA MKOPO

KLABU ya Leeds United itamruhusu pia mshambuliaji wa England, Joe Gelhardt, kwenda kwa mkopo Januari hii kwani mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ameambiwa hayuko katika mipango ya kocha Jesse March. ***(Football Insider)***

### FOREST KWA DANILO

KLABU ya Nottingham Forest ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil, Danilo mwenye umri wa miaka 21, kwa ada ya pauni milioni 18 kutoka Palmeiras. ***(Mail)***

### BUSQUETS KUTUA AL NASSR

KLABU ya Saudi Arabia ya Al Nassr inataka kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Sergio Busquets, mwenye umri wa miaka 34, ambaye mkataba wake na Barcelona utamalizika msimu wa majira ya joto. ***(ESPN)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BALE ASTAAFU RASMI SOKA

**Ninajisikia mwenye bahati sana kutimiza ndoto yangu ya kucheza mchezo ninaoupenda, kwa kweli...**

**LONDON, England**

NAHODHA wa Wales, Gareth Bale, ametangaza rasmi kustaafu soka ya ushindani kwa klabu na kimataifa.

Katika taarifa yake, Bale amesema kwamba, alichokifanya kwenye soka kinatosha na sasa ni muda wake wa kuangalia changamoto nyingine kwenye maisha.

"Ninajisikia mwenye bahati sana kutimiza ndoto yangu ya kucheza mchezo ninaoupenda. Kwa kweli imenipa baadhi ya nyakati bora zaidi za maisha yangu. Viwango vya juu zaidi ya misimu 17, ambayo haitawezekana kujirudia, haijalishi sura inayofuata imeniandalia nini," alisema katika waraka wake.

"Kuanzia mwanzo wangu kule Southampton hadi mwisho wangu na LAFC na kila kitu katikati, viliunda maisha yangu ya soka la klabu, ambalo ninajivunia sana na kushukuru. Kuichezea na kuiongoza nchi yangu mara 111 imekuwa ndoto ya kweli.

"Kuonyesha shukrani zangu kwa wale wote ambao wameshiriki sehemu yao katika safari hii, ninahisi kama jambo lisilowezekana. Ninahisi kuwa na deni kwa watu wengi waliosaidia kubadilisha maisha yangu na kuunda kazi yangu ya soka kwa njia ambayo sikuwahi kufikiria nilipoanza nikiwa na umri wa miaka 9.

"Kwa Klabu zangu za awali, Southampton, Tottenham, Real Madrid na hatimaye LAFC. Wasimamizi na makocha wangu wote wa awali, wafanyakazi wa timu, wachezaji wenzangu, mashabiki wote waliojitolea, mawakala wangu, marafiki na familia yangu, wamekuwa na mchango mkubwa usiopimika.

"Wazazi wangu na dada yangu, bila kujitolea kwenu katika siku hizo za mwanzo, bila msingi imara kama huu, nisingekuwa nikiandika taarifa hii hivi sasa, kwa hiyo asanteni kwa kuniweka kwenye njia hii na kwa msaada wenu usio na shaka.

"Mke wangu na watoto wangu, upendo wako na msaada wako umenibeba. Kando yangu katika hali zote; kupanda na kushuka, ukiniwekea msingi imara katika safari hii. Unanitia moyo kuwa bora na kukufanya uwe na fahari. Ni wakati wa mabadiliko na mpito, fursa ya tukio jipya."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,065,5

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 11,12 NA 13 JANUARI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/01/23 | 20:00 | AEL Limassol vs Apollon Limassol | 2.73 | 3.22 | 2.37 |
| 02. 11/01/23 | 20:00 | Kortrijk vs Mechelen | 2.62 | 3.41 | 2.44 |
| 03. 11/01/23 | 21:00 | Nantes vs Lyon | 3.22 | 3.31 | 2.19 |
| 04. 11/01/23 | 21:00 | AJ Auxerre vs Toulouse | 2.64 | 3.29 | 2.54 |
| 05. 11/01/23 | 21:00 | AC Ajaccio vs Reims | 2.90 | 3.10 | 2.46 |
| 06. 11/01/23 | 22:00 | VVV Venlo vs Emmen | 3.05 | 3.49 | 2.17 |
| 07. 11/01/23 | 22:45 | Nottingham vs Wolverhampton | 2.63 | 3.12 | 2.68 |
| 08. 12/01/23 | 02:00 | Alebrijes De Oaxaca vs Club Celaya | 2.60 | 3.15 | 2.75 |
| 09. 12/01/23 | 04:05 | Cancun FC vs Leones Negros Udg | 2.63 | 3.07 | 2.53 |
| 10. 12/01/23 | 18:00 | Ghazl EL Mahallah vs Enppi Club | 2.65 | 2.65 | 3.15 |
| 11. 12/01/23 | 20:45 | Heracles Almelo vs GO Ahead Eagles | 2.21 | 3.51 | 2.96 |
| 12. 12/01/23 | 22:45 | Union Saint Gilloise vs KAA Gent | 2.24 | 3.45 | 3.10 |
| 13. 13/01/23 | 11:45 | Macarthur FC vs Central Coast Mariners | 2.47 | 3.28 | 2.74 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa · vodacom m-pesa · halopesa · airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# FIFA, PSG, ETO'O NA SONG WALIMLILIA MODESTE M'BAMI

**LE HAVRE, Ufaransa**

KOCHA Mkuu wa Cameroon, Rigobert Song amesema "mdogo wangu" Modeste M'Bami alikuwa "mchezaji mwenye furaha na kipaji kikubwa" baada ya kifo cha mchezaji huyo wa zamani wa 'Simba Wasiofugika' akiwa na umri wa miaka 40.

Kiungo huyo wa zamani wa Paris St-Germain na Marseille, alifariki dunia baada ya kupata mshtuko wa moyo jijini Le Havre nchini Ufaransa, Jumamosi.

Song alicheza pamoja na M'Bami kwenye kikosi cha Cameroon na wote walikuwa sehemu ya timu iliyofika fainali ya Kombe la Shirikisho la Fifa 2003 nchini Ufaransa.

Ilikuwa ni mchuano uliogubikwa na kifo cha kiungo Marc Vivien Foe kutokana na matatizo ya moyo wakati wa mchezo wa nusu fainali na Colombia mjini Lyon.

"Nitahifadhi ucheshi wako mzuri, kipaji chako na furaha yako ya kuishi nami. Pumzika kwa amani mdogo wangu," alisema Song, ambaye alikuwa nahodha wakati M'Bami alipocheza katika mechi zote tano kwenye mashindano ya 2003 nchini Ufaransa.

M'Bami, ambaye alianza soka lake la Ulaya akiwa katika klabu ya Sedan, aliichezea nchi yake mara 38 katika ngazi ya juu, akifunga mabao matatu.

Atakumbukwa kwa bao lake la kuvutia la robo fainali dhidi ya Brazil kwenye michezo ya Olimpiki ya Sydney mwaka 2000 nchini Australia kabla ya Cameroon kunyakua medali ya dhahabu.

M'Bami alimaliza soka lake katika Klabu ya Le Havre mwaka 2016, akiwa amewahi kucheza nchini Hispania, China, Saudi Arabia na Colombia.

Kwenye chapisho la Instagram saa chache baada ya kifo cha M'Bami kuthibitishwa, rais wa Fifa, Gianni Infantino, aliweka picha ya kiungo huyo na kuandika "habari ya huzuni, RIP Modeste M'Bami".

Rais wa Shirikisho la Soka la Cameroon, Samuel Eto'o, ambaye alicheza pamoja na M'Bami wakati nchi hiyo iliponyakua dhahabu ya Olimpiki mwaka 2000, aliandika: "Umeondoka mapema sana."

Mshambuliaji wa zamani wa Cameroon, Patrick Mboma, alisema: "Si wewe Modeste, inasikitisha sana. Wewe ni Simba milele."

Shirikisho la Soka barani Afrika (Caf), lilisema "tunatoa salamu za rambirambi kwa familia ya M'Bami na familia ya soka ya Cameroon wakati huu mgumu".

Kiungo wa zamani wa PSG, Liverpool na Mali, Mohamed Sissoko alisema: "Maneno hayatoshi kueleza masikitiko makubwa ninayopata kwa kuondokewa na Modeste M'Bami. Ninatoa rambirambi zangu kwa familia yake yote."

# Lloris abwaga manyanga Ufaransa

**LONDON, England**

GOLIKIPA na nahodha wa Ufaransa, Hugo Lloris, amestaafu kucheza soka la kimataifa baada ya kuiongoza nchi yake kutinga fainali ya pili mfululizo ya Kombe la Dunia.

Lloris ndiye mchezaji aliyeichezea mechi nyingi zaidi 'Les Bleus' na amekuwa nahodha wa timu hiyo tangu mwaka 2012.

Mchezaji huyo wa Tottenham Hotspur, aliwahi kuwa nahodha wa nchi yake kwenye michuano sita mikubwa, ikiwa ni pamoja na Kombe la Dunia mara tatu.

Lloris ndiye aliyekuwa nahodha wakati Ufaransa ikishinda taji lao la pili la dunia mwaka 2018, baada ya kupoteza katika fainali ya michuano ya Euro 2016 ya nyumbani miaka miwili iliyopita.


Pia, Lloris alikuwa na kikosi cha Ufaransa kwenye fainali ya Kombe la Dunia kule Qatar 2022, na kupoteza kwa mikwaju ya penalti kutoka kwa Argentina.

Baada ya kuchukua muda kutangaza uamuzi kutokana na kushindwa huko, Lloris alithibitisha kustaafu kwake katika mahojiano na L'Equipe jana.

"Kuna wakati inabidi ujue jinsi ya kukabidhi," alisema.

"Sitaki kumiliki (nafasi hiyo). Nimekuwa nikisema na kurudia mara kwa mara kwamba timu ya Ufaransa si mali ya mtu yeyote, na sote tunapaswa kuhakikisha kuwa hilo.

"Nadhani bado kuna timu iliyo tayari kuendelea, na pia kuna kipa ambaye yuko tayari."



505,647/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/01/23 | 18:00 | Nottingham Forest vs Leicester City | 2.80 | 3.30 | 2.46 |
| 02. 14/01/23 | 18:00 | Wolverhampton Wanderers vs West Ham United | 2.65 | 3.20 | 2.65 |
| 03. 14/01/23 | 18:00 | Luton Town vs West Bromwich Albion | 2.95 | 3.20 | 2.40 |
| 04. 14/01/23 | 18:00 | Preston North End vs Norwich City | 2.95 | 3.25 | 2.38 |
| 05. 14/01/23 | 18:00 | Reading FC vs Queens Park Rangers | 2.46 | 3.25 | 2.80 |
| 06. 14/01/23 | 18:00 | Sunderland AFC vs Swansea City | 2.49 | 3.25 | 2.75 |
| 07. 14/01/23 | 18:00 | DR Congo vs Uganda | 2.39 | 2.75 | 3.45 |
| 08. 14/01/23 | 18:15 | Girona FC vs Sevilla FC | 2.40 | 3.25 | 2.90 |
| 09. 14/01/23 | 20:15 | KAS Eupen vs St. Truidense VV | 2.80 | 3.35 | 2.42 |
| 10. 14/01/23 | 20:45 | FC Volendam vs RKC Waalwijk | 2.65 | 3.50 | 2.46 |
| 11. 14/01/23 | 21:00 | Ivory Coast vs Senegal | 2.85 | 2.95 | 2.65 |
| 12. 14/01/23 | 23:00 | Real Sociedad San Sebastian vs Athletic Bilbao | 2.50 | 3.15 | 2.80 |
| 13. 15/01/23 | 16:00 | Getafe CF vs Espanyol Barcelona | 2.50 | 2.95 | 2.95 |
| 14. 15/01/23 | 16:30 | Go Ahead Eagles vs FC Utrecht | 2.80 | 3.50 | 2.35 |
| 15. 15/01/23 | 17:00 | Angers SCO vs Clermont Foot 63 | 2.42 | 3.40 | 2.75 |
| 16. 15/01/23 | 17:00 | Montpellier HSC vs FC Nantes | 2.45 | 3.40 | 2.70 |
| 17. 15/01/23 | 17:00 | Stade Reims vs OGC Nice | 2.55 | 3.20 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 11/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 4746 | Nikolaos vs Apollon Paralimniou | 1.73 | 3.46 | 4.28 |
| 15:10 | 2002 | Hajer Club vs Najran SC | 2.17 | 2.92 | 3.36 |
| 15:25 | 5312 | AL Hazm vs AL Arabi (SA) | 1.96 | 3.16 | 3.65 |
| 15:45 | 2287 | El Daklyeh vs National Bank | 4.18 | 2.94 | 2.02 |
| 15:45 | 2732 | AL Akhdood vs AL Sahel SC | 2.03 | 2.97 | 3.70 |
| 15:45 | 5495 | Smouha Club vs Talaea El Gaish | 2.48 | 2.73 | 3.27 |
| 16:00 | 3980 | JSM Tiaret vs RC Kouba | 1.37 | 4.18 | 7.59 |
| 16:30 | 2789 | Rajasthan United vs Sreenidi Deccan FC | 2.48 | 3.16 | 2.63 |
| 16:30 | 5430 | Cape Town All Stars vs Mm Platinum FC | 1.89 | 2.95 | 5.00 |
| 17:00 | 2357 | Vilaverdense FC vs Belenenses | 2.06 | 3.30 | 3.21 |
| 17:00 | 3333 | Aris Salonica vs Levadiakos | 1.33 | 4.37 | 8.35 |
| 17:30 | 5804 | Volos vs Panathinaikos | 4.88 | 3.61 | 1.62 |
| 18:30 | 1396 | Al Rayyan SC vs Al Sadd SC | 5.65 | 4.87 | 1.39 |
| 18:30 | 5572 | Qatar SC vs Al Gharafa SC | 3.17 | 3.31 | 2.07 |
| 20:00 | 1042 | El Ittihad Alexandria vs Zamalek | 4.09 | 3.34 | 1.88 |
| 20:00 | 1977 | Nea Salamis vs AEK Larnaca | 4.18 | 3.45 | 1.75 |
| 20:00 | 3150 | AEK Athens vs Kifisias | 1.07 | 7.78 | 27.23 |
| 20:00 | 4617 | Coca Cola vs Pyramids | 3.94 | 3.14 | 1.99 |
| 20:00 | 5609 | AEL Limassol vs Apollon Limassol | 2.73 | 3.22 | 2.37 |
| 20:30 | 1824 | Nacional Madeira vs Rabo De Peixe | 1.41 | 4.39 | 6.05 |
| 20:30 | 3663 | Stellenbosch vs Marumo Gallants FC | 2.30 | 2.83 | 3.42 |
| 20:30 | 5893 | Kortrijk vs Mechelen | 2.62 | 3.41 | 2.44 |
| 20:45 | 3743 | SBV Excelsior vs AZ Alkmaar | 5.83 | 4.57 | 1.41 |
| 21:00 | 1336 | Clermont Foot vs Rennes | 3.78 | 3.48 | 1.91 |
| 21:00 | 1353 | AJ Auxerre vs Toulouse | 2.68 | 3.27 | 2.53 |
| 21:00 | 1827 | Nantes vs Lyon | 3.19 | 3.28 | 2.19 |
| 21:00 | 3393 | AC Ajaccio vs Reims | 2.98 | 3.08 | 2.41 |
| 21:00 | 4744 | Brest vs Lille | 3.70 | 3.50 | 1.93 |
| 21:45 | 5206 | Sporting Braga vs Vitoria Guimaraes | 1.49 | 4.09 | 5.45 |
| 22:00 | 2432 | De Treffers vs Cambuur | 3.99 | 3.80 | 1.70 |
| 22:00 | 3469 | Almere City vs NEC Nijmegen | 3.01 | 3.40 | 2.11 |
| 22:00 | 3772 | Atromitos vs Olympiakos | 4.77 | 3.55 | 1.64 |
| 22:00 | 3813 | VVV Venlo vs Emmen | 2.97 | 3.41 | 2.13 |
| 22:00 | 4645 | Real Madrid vs Valencia | 1.51 | 4.17 | 5.76 |
| 22:00 | 5114 | Heerenveen vs FC Volendam | 1.53 | 4.20 | 4.78 |
| 22:00 | 5473 | Zulte Waregem vs St Truiden | 3.10 | 3.50 | 2.10 |
| 22:30 | 4755 | CP Cacereno vs CD Coria | 2.02 | 3.17 | 3.46 |
| 22:45 | 1280 | Nottingham vs Wolverhampton | 2.58 | 3.12 | 2.73 |
| 22:45 | 3295 | Queens Park vs Raith Rovers | 1.85 | 3.60 | 3.55 |
| 22:45 | 4048 | Racing Genk vs Royal Antwerp | 1.86 | 3.66 | 3.66 |
| 23:00 | 2397 | Strasbourg vs Lens | 3.64 | 3.39 | 1.98 |
| 23:00 | 2827 | Lorient vs Monaco | 3.64 | 3.68 | 1.89 |
| 23:00 | 3191 | Den Bosch vs Ajax | 22.45 | 9.37 | 1.05 |
| 23:00 | 3591 | AC Milan vs Torino | 1.57 | 3.94 | 5.38 |
| 23:00 | 4334 | Paris St Germain vs Angers | 1.14 | 7.59 | 15.16 |
| 23:00 | 5835 | Troyes vs Marseille | 4.59 | 3.89 | 1.67 |
| 23:00 | 5899 | Nice vs Montpellier | 1.79 | 3.60 | 4.20 |
| 23:00 | 5972 | Southampton vs Manchester City | 9.88 | 5.39 | 1.27 |
| 23:15 | 1465 | Viseu vs SC Beira Mar | 1.43 | 4.37 | 5.83 |
| 23:45 | 4448 | Porto vs FC Arouca | 1.11 | 7.38 | 16.50 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# BARES ATOA SIRI MLANDEGE KUZICHAPA TIMU ZA BARA

**Na Saada Akida, Zanzibar**

WAKATI timu ya Mlandege ikijiandaa kuivaa Singida Big Stars katika mchezo wa fainali ya Kombe la Mapinduzi utakaopigwa katika Uwanja wa Amaan, visiwani hapo keshokutwa, Ijumaa, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdallah Mohamed 'Bares', ametoa siri ya kikosi chake kuzifunga timu za Tanzania Bara.

Mlandege FC imetinga fainali baada ya kuitupa nje Namungo FC katika hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo juzi usiku kwa mikwaju ya penalti 4-3 kutokana na dakika 90 kumalizika timu hizo zikitoshana nguvu kwa kufungana bao 1-1, Uwanja wa Amaan.

Hii ni mara ya kwanza baada ya miaka 11 kwa timu kutoka Zanzibar kutinga fainali ya Kombe la Mapinduzi kwani mara ya mwisho ilikuwa mwaka 2012, Jamhuri ilipocheza dhidi ya Azam FC ambyo ilitwaa taji hilo kwa kuibuka na ushindi wa mabao 3-1.

Kabla ya kuiondoa Namungo FC hatua ya nusu fainali, Mlandege ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya KVZ na kisha kuichapa Simba bao 1-0, hivyo kuwa timu pekee iliyopo katika mashindano hayo kati ya sita zilizoshiriki.

Kwa upande wa Namungo yenyewe ilifuzu kimiujiza mbele ya Aigle Noir iliyonyimwa penalti mbili za wazi ikiing'oa Chipukizi ya Pemba iliyokuwa ikiongoza Kundi D.

Mlandege ambayo imefanikiwa kuingia fainali kwa mara ya kwanza katika misimu 17 ya michuano hiyo, pia inataka kuzivua joho la unyonge timu za Zanzibar ikitaka kubeba taji.

Akizungumzia mchezo huo wa nusu fainali dhidi ya Namungo FC, Bares alisema uzoefu alioupata katika timu za Tanzania Bara alizokuwa akizifundisha umesaidia kuiwezesha Mlandege kufikia malengo hayo ya kucheza fainali.

"Tumefanikiwa kucheza fainali na nitafanyia kazi mapungufu ya kikosi changu, kujiandaa na mchezo wetu wa fainali dhindi ya Singida Big Stars," alisema Bares.

Alisema timu yake imejiandaa vizuri kwa mechi hiyo licha ya kutambua ugumu atakaokutana nao uwanjani dhidi ya wapinzani wao, Singida Big Stars ambao wanacheza nao fainali.

"Nina watu wengi nyuma yangu ambao wananiangalia ni kwa namna gani nitaipambania Zanzibar kutwaa ubingwa. Wachezaji wangu wapo fiti na wana morali ya kuhakikisha wanafanya vizuri na hatimaye kubakiza kombe hili," alisema Bares.

Kocha Mkuu wa Namungo FC, Denis Kitambi, amekiri mechi ilikuwa na ushindani mkubwa na bahati haikuwa kwao hivyo kuondolewa katika mashindano hayo.




Rais wa Heshima wa Simba na Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji, akisalimiana na Kiungo mpya timu hiyo, Saido Ntibazonkiza, baada ya kukutana na kuzungumza na wachezaji pamoja na benchi la ufundi katika kambi yao huko Dubai jana. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA KUVAANA NA CSKA MOSCOW

INATOKA UK. 24

3, mwaka huu.

Baada ya mechi hiyo, ataingia kwenye kazi yenyewe inayotupiwa jicho na Wanasimba wengi kwa kuiongoza kwenye mechi ya kwanza ya hatua ya Makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika ugenini nchini Guinea dhidi ya wenyeji wao, Horoya AC.

Wakati huo huo, Rais wa Heshima na Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji, amemweleza Robertinho na wachezaji wa klabu hiyo kuwa nia yake ni siku moja kuona Simba inafanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa barani Afrika.

Mo alitoa kauli hiyo baada ya kutembelea kambi ya timu hiyo mjini Dubai jana na kuwaeleza kuwa kila kitu kitawezekana endapo tu watafanya jitihada katika mechi zao.

Hata hivyo, amewataka kabla ya kuchukua ubingwa wa Afrika, wachezaji wapambane ili kuhakikisha wanarejesha taji lao la Ligi Kuu na Kombe la FA.

Katika msimamo wa Ligi Kuu, Simba ipo nafasi ya pili ikiwa na pointi 44, sita nyuma ya Yanga iliyoko kileleni baada ya timu zote kucheza mechi 19 hadi sasa msimu huu.

# Michezo

Jumatano Januari 11, 2023

Nipashe




UKURASA 21

## Bale astaafu rasmi soka

'WALETE WAZUNGU'...




Kikosi cha CSKA Moscow, kinachotarajiwa kuvaana na Simba katika mechi ya kirafiki itakayopigwa Abu Dhabi, Falme za Kiarabu Jumapili wiki hii. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA KUVAANA NA CSKA MOSCOW

●●●Ni wazoefu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na Europa League, Mo Dewji atembelea kambi Dubai atoa neno...

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba ambacho kiko kambini huko Dubai, Falme za Kiarabu, kikijiandaa na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Ligi Kuu, Jumapili wiki hii kinatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya klabu kubwa nchini Urusi, CSKA Moscow, ambayo imekuwa ikishiriki mara kwa mara Ligi ya Mabingwa Ulaya na michuano ya Europa League, imeelezwa.

Simba ambayo imeweka kambi ya wiki moja huko, itacheza mechi hizo kwenye mji wa Abu Dhabi ambao ni wa pili kwa ukubwa ukiacha Dubai ambako imepiga kambi yake.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo imeeleza kuwa, kabla ya mechi hiyo ya Jumapili, keshokutwa Ijumaa itakipiga dhidi ya Al Dhafra ya Falme za Kiarabu kwenye mji huo huo wa Abu Dhabi.

Mechi hizo zote zitachezwa majira ya saa 11:00 kwa saa za huko ambazo ni saa 10:00 jioni kwa saa za Afrika Mashariki.

CSKA Moscow ilioanzishwa mwaka 1911, ni timu maarufu sana hasa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Europa League ambapo imekuwa ikishiriki mara kwa mara.

Kwa sasa inashika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu nchini Urusi, ikiwa na pointi 29 kwa michezo 17 iliyocheza mpaka sasa, ikishinda mechi nane, sare tano na kupoteza nne.

Imetwaa ubingwa wa Ligi Kuu Urusi mara 13, mara ya mwisho ikiwa ni msimu wa 2017/18 na mafanikio yake makubwa Ulaya ni kutwaa Kombe la UEFA msimu wa 2004/05 na kufika fainali ya UEFA Super Cup 2005.

Al Dhafra ambayo inashiriki Ligi Kuu ya Falme za Kiarabu yenye timu 14, kwa sasa, inakamata mkia ikiwa na pointi nne tu, kwa mechi 12 ilizocheza, ikishinda moja, sare moja na kupoteza 10. Timu hiyo ilianzishwa mwaka 2000.

Simba inaitumia kambi hiyo na mechi hizo za kirafiki ili kumpa nafasi nzuri Kocha Mkuu mpya, Robertinho Oliveira, aliyejiunga na timu hiyo mapema mwezi huu, kutambua uwezo wa kila mchezaji pamoja na kuwaongezea mbinu kabla ya kurejea kwenye Ligi Kuu Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika mwezi ujao.

Robertinho ataanza kukiongoza kikosi chake kwa mara ya kwanza kwenye mechi za mashindano akiwa na Simba itakapoikaribisha Mbeya City kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumanne ijayo kabla ya kuifuata Dodoma Jiji Januari 22 na kisha kurejea Dar es Salaam kuvaana na Singida Big Stars Februari

INAENDELEA UK. 23

## Yanga yafunguka usajili wao mpya

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Yanga waliokuwa na kikosi hicho kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi wanatarajia kurejea kambini keshokutwa, Ijumaa huku klabu hiyo ikikanusha kuwa kwenye mpango wa kuwasajili wachezaji Thomas Ulimwengu na Kazadi Kasengu.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema amekuwa akiona na kusikia baadhi ya wachambuzi na kwenye mitandao ya kijamii kuwa wana nia ya kuwasajili wachezaji hao kitu ambacho si kweli kwa sababu hawapo kwenye mipango yao.

"Hiyo niweke wazi kabisa, ni kweli kuna wachezaji wawili tunawasajili na tutawatangaza siku hizi mbili tatu kabla ya kufungwa dirisha dogo la usajili lakini siyo Ulimwengu wala Kazadi, kwa sababu kule kwenye Kombe la Mapinduzi baada ya huyo jamaa kuwafunga Azam FC kumekuwa na stori nyingi zikituhusisha kumsajili. Nachoweza kusema kuwa hawa wote ni wachezaji wazuri sana, tunawaheshimu, lakini hawakuwa kwenye mipango yetu na kwa kuwaonyesha kwamba si kweli, sisi hatusajili mastraika wawili, tunasajili straika mmoja na beki wa kati mmoja," alisema Kamwe.

Ulimwengu mchezaji wa kimataifa wa Tanzania na Kazadi aliyekiwasha kwenye mechi za Kombe la Mapinduzi akiwa na Singida Big Stars, wote ni mastraika.

Alisema baada ya kumsajili Mudathir Yahaya na kufanya vema kwenye Kombe la Mapinduzi, wanamalizia na wachezaji wawili ambao ni wakubwa na wanatoka kwenye klabu kubwa.

"Ni wachezaji wanaotoka moja kwa moja kwenye mashindano katika nchi zao, dirisha hili ni lazima utafute mchezaji ambaye anacheza na ukimwongeza anaingia moja kwa moja kwenye kikosi. Hawa ni wachezaji wakubwa, wanatoka klabu kubwa," alisema.

Straika anayetajwa sana kuwa kwenye hatua za mwisho kujiunga na Yanga ni Kennedy Musonda kutoka Power Dyanamos ya Zambia.

Kamwe alisema baada ya kuondolewa kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi, kesho wanaingia kambini kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Ihefu FC itakayopigwa Jumatatu ijayo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002